**Ziara** Majaliwa yang'oa maofisa wanne wa TRA
UKURASA 4



**Ajali** ya lori, basi yakatisha uhai watu kumi na kujeruhi 22
UKURASA 3



**Mahakama**: Hakuna Sheria iliyovunjwa kuhusu Jaji Mkuu
UKURASA 4


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Septemba 24, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581443

www.ippmedia.com



tigo pesa SportPesa

MAOKOTO Deilee!

WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




UKURASA 9

# DK. Shoo afunguka magumu aliyopitia uongozi KKKT

• **Aeleza** ali-choteta na Rais kwa ustawi wa taifa... *Endelea Ukurasa 2*



Askofu Dk. Fredrick Shoo

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### EWURA, LATRA ZAONYA UPANDISHAJI WA NAULI

BAADHI ya wasafirishaji mkoani Tabora, wamedaiwa kupandisha nauli kinyemela kwa kile kinachodaiwa kuwa ni kutokana na ongezeko la bei ya mafuta ambako kwa mkoa huo lita ya petroli imepanda kwa Sh...

UKURASA WA 5

### TUME YA SHERIA YAKABIDHI RIPOTI KWA WAZIRI

TUME ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT) imewasilisha ripoti mbili za mapitio ya mfumo wa sheria unaosimamia makosa dhidi ya maadili na taarifa ya mapitio ya ...

# Panga la Samia lilivyofyeka vigogo TANESCO, Mtwara

UK. 2



Mkurugenzi Mtendaji mpya TANESCO, Mhandisi Gissima Nyamo-Hanga.



Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji TANESCO, Maharage Chande.



Mwenyekiti mpya bodi ya TANESCO, Meja jenerali Paul Simuli.



Aliyekuwa Mwenyekiti bodi ya TANESCO, Omary Issa.

# Waziri ashangaa 'ambulance' kubeba maofisa halmashauri

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA YAIFUNGIA KAZI DYNAMOS UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni cha Urusi, Alexey Bondaruk akitoa maelezo kwa baadhi ya wananchi waliojitokeza katika tamasha la kidini lililoandaliwa na kituo hicho, jijini Dar es Salaaam juzi. Wa (tatu kulia) ni Shekhe Mussa Kundecha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Askofu Shoo afunguka magumu aliyopitia katika uongozi KKKT

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amesema katika kipindi chake cha uongozi wa kanisa hilo, amepitia mengi ya baraka, na mengine magumu sana.

Dk. Shoo ambaye ni Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini, amesema katika kipindi hicho ameimarika zaidi katika utumishi wake.

Hata hivyo, amesema moja ya matukio yaliyomsikitisha sana ni lile la Askofu mmoja wa KKKT kumtuhumu kuwa alipokwenda Ikulu kukutana na Rais Samia Suluhu Hassan, hakufanya kitu kingine zaidi ya kumwomba Rais ampe gari.

Askofu Dk. Shoo alisema hayo jana nyumbani kwake, Mailisita, Hai mkoani Kilimanjaro, wakati wa ibada ya shukrani ya kupewa gari la kifahari aina ya Toyota Land Cruiser GR Spot lenye thamani ya Sh. milioni 500.

Gari hilo lenye namba za usajili T 444 EEY rangi nyeusi, limenunuliwa na marafiki 62 wa Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Kijitonyama, Dar es Salaam, Dk. Eliona Kimaro, ambao ni wafanyabiashara na wanasiasa.

"Mimi nimetindikiwa hata sijui niseme nini. Huu ni uthibitisho wa nguvu ya upendo. Asanteni kwa upendo katika jambo hili mlilonionyesha katika tendo hili.

"Ndugu zangu, Mungu amenisaidia nimemaliza kipindi changu cha ukuu wa kanisa. Nimepitia mengi ya baraka, mengine magumu sana kama wengine walivyoelezea hapa. Lakini katika yote nimemwona Bwana (Mungu) akinishika kwa mkono wake na hapa niseme tu katika kipindi hicho, nimeimarika zaidi katika utumishi wangu.

Katika kipindi chote hicho, Mungu amejidhihirisha kwangu. Natambua kama kuna jema lolote nililolifanya, ni kwa msaada wa Mungu," alisema.

**TUKIO ANALOLIKUMBUKA**

Askofu Dk. Shoo katika hotuba yake, alisema: "Mtakuwa mnakumbuka 4/3/2022, mnajua nini kilitokea kama mna kumbukumbu. Ndugu yetu ambaye pia Mungu amemleta yuko hapa, Freeman Mbowe, aliyekuwa ameshikiliwa ndani kwa muda mrefu ndio alipoachiwa.

"...Kwamba Mungu alinitumia kwa namna gani hilo analijua yeye. Lakini kwa njia ya ajabu tu tulipata nafasi ya kukaa na Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia. Si mara moja, si mara mbili, si mara tatu kuhusu jambo la huyu ndugu yetu na wale wengine."

Kutokana na kukutana na kiongozi huyo wa nchi, mkuu huyo wa KKKT, alisema Rais Samia kwa moyo wake alilipokea jambo hilo.

Alisema kilichoendelea baada ya hapo, tena baada ya muda, ndipo alipopelekewa taarifa na Mchungaji mmoja, akimwambia: "Baba, mbona kuna Askofu mwenzako, anasema ulipoenda kule Ikulu wewe hukufanya kitu kingine zaidi ya kumwomba mama Samia akupe gari?"

Kwa mujibu wa Askofu Dk. Shoo, Askofu huyo aliyemtuhumu wakati anawaambia, kulikuwa na mkutano wa wasaidizi wa Maaskofu.

"Nafikiri ilikuwa kule Mwanza. Askofu Shoo, unafikiri ameenda kufanya chochote huko, ameenda kumwomba Rais gari.

"Nilipopata taarifa hizi nilisikitika sana lakini nikamwambia Mungu wewe unajua. Katika utumishi huu, katika mambo niliyokuomba na kwa nafasi uliyonipa nisitafute faida yangu binafsi. Nisaidie Mungu niwatumikie hawa watu ulionipa kwa uaminifu."

Baada ya tuhuma hiyo kuelekezwa kwake, Askofu Dk. Shoo alisema sauti ilimwambia: "Fred, usijali mwanangu. Ndiyo neno tu, usijali."

"Wanasiasa mko hapa mtasingiziwa, wakati mwingine mnaweza mkafanyiana mambo ya ajabu ajabu huko. Lakini napenda kuwaambia simameni na Mungu. Uaminifu wa Mungu ni wa milele kwa wale wote wanaomcha," alisema.

**MBOWE ATOA DUKUDUKU**

Mmoja wa watu waliofanikisha kununuliwa gari hilo, Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, alimwomba Dk. Shoo kuliongoza kanisa kusimamia na kulilinda taifa.

"Kanisa limetuunganisha, kanisa limetupa huduma. Baba Askofu endeleeni kusimamia na kuilinda haki katika nchi yetu. Katika taifa letu na katika dunia. Wala kanisa la Mungu lisisite kusema ukweli. Kanisa la Mungu ni ukweli na ukweli hautapindishwa wakati mwingine wowote.

"Nikitazama kushoto nawaona viongozi wa CCM. Nikitazama kulia sioni viongozi wa CHADEMA. Naogopa niseme nini ambao ndugu zangu hawa watakuwa na amani. Nilipokuja hapa nilimwomba sana Mungu anipe kibali.

"Jambo hili limetuweka pamoja kama watoto wa Kristo. Chini ya Mchungaji Eliona Kimaro hatutajadili mambo ya kiitikadi na wala hatutajadili. Tunazungumza maisha yetu ya kiroho," alisema.

# Panga la Samia lilivyofyeka vigogo TANESCO, Mtwara

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameendelea kufanya mabadiliko katika serikali na taasisi zake kwa kufanya uteuzi na kutengua baadhi ya viongozi na watendaji katika wizara, mikoa na wilaya.

Mabadiliko hayo yaliyofanywa na Rais na kutangazwa jana asubuhi, yamehusu pia uongozi wa juu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambalo kwa sasa linakabiliwa na changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara pamoja na Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL).

Uteuzi na utenguzi huo uliofanywa umeugusa pia mkoa wa Mtwara kwa kutenguliwa kwa katibu tawala wa mkoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri zikiwa ni siku chache baada ya Rais kufanya ziara ya kikazi mkoani humo.

Katika ziara hiyo, Rais alibaini kuwapo kwa madudu mbalimbali ukiwamo utendaji usioridhisha kwa baadhi ya wateule wake na kuahidi kuchukua hatua. Hata hivyo, haikuelezwa kama hatua inatokana na madudu hayo.

Pia mabadiliko ya TANESCO na TTCL hayakubainishwa kama yanatokana na kilio cha wananchi cha sasa kuhusu kero ya upatikanaji wa nishati hiyo ambayo sasa iko kwa mwendo wa mgawo, ambao shirika limesema ni ratiba ya ugavi kutokana na kuwapo kasoro za mitambo.

Aidha, kwa TTCL, licha ya kutokuwapo sababu, Rais katika mkutano wake na wakuu wa mashirika ya umma ulioandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina, alihoji shirika hilo kutotimiza majukumu yake ipasavyo, hivyo linapaswa kujitathmini.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, ilisema Rais Samia amemteua, Mhandisi Gissima Nyamo-Hanga kuwa Mkurugenzi Mtendaji mpya wa TANESCO. Mhandisi Nyamo-Hanga aliwahi kuwa Mkurugernzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Rais Samia amemteua aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, akichukua nafasi ya Mhandisi Peter Ulanga, ambaye taarifa hiyo ilisema atapangiwa kazi nyingine.

Mabadiliko hayo pia yamegusa bodi ya wakurugenzi ya TANESCO kwa Rais kumteua Meja Jenerali Paul Simuli kuwa mwenyekiti huku aliyekuwa akishika nafasi hiyo, Omar Issa, taarifa ikieleza ataendelea na majukumu mengine aliyopangiwa katika Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango.

Sambamba na taasisi hizo, nyingine iliyoguswa ni Taasisi ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kuteuliwa Mkurugenzi Mkuu mwingine ambaye ni Dk. Erasmus Kipesha. Kabla ya uteuzi huo, Dk. Kipesha alikuwa Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi ndani ya mamlaka hiyo. Anachukua nafasi ya Bahati Geuzye ambaye ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara.

**MSIGWA AULA**

Katika mabadiliko hayo pia, Rais Samia amemteua Gerson Msigwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ambapo kabla alikuwa Msemaji Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari - MAELEZO. Taarifa hiyo ilisema nafasi ya Msemaji Mkuu wa Serikali itatangazwa baadaye.

Aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo, Said Othman Yakubu, ameteuliwa kuwa balozi.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametengua uteuzi wa Abdallah Malela, Katibu Tawala Mkoa wa Mtwara na kumteua Bahati Geuzye kushika nafasi hiyo. Pia amemteua Mohamed Gombati kuwa Katibu Tawala Mkoa wa Geita ambapo kabla ya uteuzi, alikuwa Mkurugenzi Msaidizi sehemu ya Maofisa Waandamizi katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora," ilisema taarifa hiyo.

Katika mabadiliko hayo, Rais ametengua uteuzi wa Hanafi Msabaha, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mjini na badala yake, amemteua Mwanahamisi Mkunda kushika nafasi hiyo. Kabla ya uteuzi huo, Mkunda aliwahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Temeke. Pia amemteua Dk. Stephen Mwakajumilo kuwa Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Mariam Chaurembo, taarifa ilieleza kuwa atapangiwa kazi nyingine.

Kadhalika amemteua Hassan Nyange kuwa Mkurugenzi (DED) wa Mtwara TC. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Namtumbo na aliyekuwa akishika nafasi hiyo, Kanali Emmanuel Mwaigobeko, atapangiwa kazi nyingine.

Rais Samia ametengua uteuzi wa Tatu Issike, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara na kumteua Abeid Kafunda kushika nafasi hiyo. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa mwanasheria katika Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

"Amemteua Reuben Jichabu kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. Aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Erica Yegella, atapangiwa kazi nyingine.

"Rais pia amemteua Francis Mgoloka kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Namtumbo. Kabla ya uteuzi huo alikuwa Katibu Tarafa Mswaki, Kilindi Handeni. Katibu Mkuu na makatibu Tawala wa Mikoa wataapishwa Jumanne mchana Ikulu, Dar es Salaam," ilisema taarifa hiyo.

## HABARI KITAIFA

# Waziri ashangaa 'ambulance' kubeba maofisa halmashauri

**Na Mwandishi Wetu,**
MPWAPWA

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene (pichani), ameujia juu uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kwa kutumia gari la wagonjwa kwa shughuli zingine.

Badala yake, ameutaka uongozi huo kutumia gari hilo la Kituo cha Afya Rudi kwa lengo lililokusudiwa ili kusaidia kupunguza vifo vya wajawazito na wagonjwa wengine pindi linapohitajika.

Amesema ni aibu kuona gari la kubebea wagonjwa likitumika kwa ajili ya kufanyia mambo mengine huku kusudio la msingi likiwa limeachwa huku wajawazito na wagonjwa wengine mahututi wakihatarisha maisha yao.

Simbachawene alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Rudi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Shule ya Msingi ya Chilendu, Jimbo la Kibakwe, Mpwapwa mkoani Dodoma, ikiwa ni ziara yake ya kimkakati ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi.

Alisema malalamiko ya wananchi walio katika hali duni ni mengi kuhusu matumizi ya gari hilo wakati kusudio lilikuwa kuwasaidia wagonjwa walioshindwa kutibiwa katika kituo hicho cha afya kukimbizwa katika hospitali ya juu zaidi ili kuokoa maisha yao.

Simbachawene alisema muda mwingi gari hilo limekuwa likitumika kwa shughuli zingine katika halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa ambako ni mbali na kituo kiliko.

"Unakutana na gari la kubebea wagonjwa limebeba maofisa wa halmashauri ilhali huku wagonjwa wanaohitaji kusafirishwa kwa matibabu zaidi wakilazimika kukodi gari kutoka kwa watu binafsi. Jambo hili halikubaliki" alisema.



Aidha, alitaka gari hilo liwapo saa 24 katika kituo hicho cha afya badala ya kuliweka katika ofisi za halmashauri kwa madai kuwa hakuna wagonjwa wanaolihitaji.

Simbachawene aliutaka uongozi wa halmashauri kujitathmini kama upo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi kwa kuwa haiwezekani wananchi wakaachwa wanataabika na muda mwingine hupoteza maisha ilhali gari lipo ila linatumika kwa matumizi yasiyostahili.

Kwa mujibu wa wananchi, licha ya kujitahidi kutumia nguvu zao kujenga sehemu maalum ya kuhifadhia gari hilo la wagonjwa katika kituo hicho cha afya, gari hilo muda mwingi limekuwa halikai hapo.

Katika hatua nyingine, Simbachawene ametoa wito kwa wajawazito kuwahi katika vituo vya afya mara waonapo dalili za kuanza kwa uchungu ili kuepuka vifo visivyo vya lazima huku akiwasihi wauguzi kuwahudumia wagonjwa kwa upendo kama viapo vyao vinavyowataka.

# Ajali ya lori, basi yakatisha uhai watu 10 na kujeruhi 22

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU 10 wamefariki dunia na wengine 23 kujeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kutoka Nsalaga jijini Mbeya kwenda katika Mji wa Mbalizi kugongwa na lori la mafuta kwenye mteremko wa Mlima Iwambi kisha kutumbukia korongoni.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP) Benjamin Kuzaga, alisema ajali hiyo ilitokea juzi saa 11:40 jioni kwenye Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM).

Aliyataja magari yaliyohusika kwenye ajali hiyo kuwa ni lori la mafuta lenye namba za usajili BCE 9384 na tela namba ABX 8675 mali ya Kampuni ya Horn Africa Motors ya Zambia na gari la abiria lenye namba za usajili T 636 DQY aina ya Mitsubish Rosa.

Kamanda Kuzaga alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa lori hilo, Mohamed Abilah (47), raia wa Somalia, kushindwa kulimudu gari hilo kwenye mteremko mkali na kwenda kuligonga gari la abiria ambalo lilikuwa linaendeshwa na Elly Mwakalindile (41), mkazi wa Iyunga jijini Mbeya.

Alisema kati ya watu waliofariki wanaume ni watano na wanawake ni wanne na kwamba mpaka sasa maiti saba zimeshatambuliwa na mbili pekee bado hazijatambuliwa.

"Wanane walifariki (dunia) papo hapo na mmoja alifariki dunia hospitalini wakati anaendelea kupatiwa matibabu, lakini dereva wa lori tumeshamkamata na tunaendelea kumhoji na baada ya hapo tutamfikisha mahakamani," alisema Kamanda Kuzaga.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali Teule Wilaya ya Mbeya ya Ifisi, Dk. Hamis Ally, alisema walipokea maiti nane na majeruhi 25 wa ajali hiyo, lakini wengine wawili wakafariki dunia wakati anatibiwa, hivyo kufanya waliofariki dunia kufikia tisa.

Alisema alisema majeruhi wanne walipewa rufani kwenda katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya baada ya kubaini kuwa hali zao zilikuwa mbaya zaidi.

Alisema katika hospitali hiyo walibaki majeruhi 20 ambao baadhi yao walitibiwa na kuruhusiwa kurudi nyumbani na baadhi ambao hali zao zilikuwa zinahitaji uangalizi wanaendelea na matibabu.

"Majeruhi wote tuliobaki nao hapa hali zao zinaendelea vizuri, wale ambao walikuwa na hali mbaya tumewapatia rufaa kwenda hospitali ya Kanda kwa matibabu zaidi," alisema Dk. Hamis.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Dennis Mwile, aliwataka madereva na wamiliki wa magari kuhakikisha wanayafanyia matengenezo ili kuepusha ajali.

Aliwapongeza wananchi wa mji wa Mbalizi ambao walijitokeza kwenda kuokoa abiria wa gari hilo pamoja na madaktari wa hospitali ya Ifisi kwa kuwahudumia vizuri wagonjwa hao.

Baadhi ya wananchi waliomba serikali kutekeleza haraka mradi wa upanuzi wa Barabara ya TANZAM na kuifanya kuwa ya njia nne kwa maelezo kuwa eneo hilo lina mteremko mkali lakini barabara ni nyembamba.

Mmoja wa wananchi hao, Boniface Mwampagama, alisema mkandarasi wa barabara hiyo amefyeka miti yote kwenye eneo hilo ambayo ilikuwa inasaidia kunusuru ajali lakini kazi ya ujenzi wa miundombinu haiendelei.

Alisema barabara hiyo ikikamilika ajali ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu zitapungua na hivyo kuruhusu wananchi kuendelea na shughuli zao kwa amani.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe: 23/09/2023

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumapili tarehe 24-09-2023** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **MTWARA**, Gari hilo lenye namba za usajili: **T 175 DFN/T 168 DFN**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **18:00** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.80** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.00** |

3. Njia itakayotumika **DAR ES SALAAM hadi MTWARA kupitia KILWA ROAD.** Gari itasafiri muda wa mchana tu ***( kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakao jitokeza.***

**KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI**

**BANSAL TRANSPORT LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 413 ACW** yenye Chassis namba **04343552.t413.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 608 ABM** yenye Chassis namba **1204476.t608** zote aina ya SCANIA. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/2868/2023.**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**HANCE JOSEPH DANIEL** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **HAOJUE** yenye jina la umiliki **GS GROUP LIMITED,** usajili namba **MC 691 CYK ,** CHASSIS NAMBA: **LC6PCJK25M0055393** na ENGINE NAMBA: **156FMI5AD3F01881.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA:**PHQ/ARU/ARU/2902/2023**

**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**MOHAMMED MABROUK MUTRIB** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE144816** iliyotolewa mwaka 2019 PCO ZANZIBAR.kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/16738/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI/TARAKA/MIRATHI NAMBA......189/2023**

**MDAI:RAMADHANI OMARY SHAWEJI**

**MDAIWA:RIDHIWANI OMARY SHAWEJI**

**KWA: RIDHIWANI OMARY SHAWEJI**
**CHAMAZI DAR ES SALAAM**
- **OMBI LA MDAI:RAMADHANI OMARY SHAWEJI**
- **MADAI YA PESA YA TSHS.16000000/=**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 16 mwezi oct Mwaka 2023 Saa 2:30 Asubuhi/alasiri.
Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmnepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa
Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 15 mwezi 09 mwaka 2023

..............................................
**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**MOROGORO**

# Ziara ya Majaliwa yasomba maofisa TRA

**Na Waandishi Wetu**

BAADA ya kuacha machungu na maumivu kwa baadhi ya maofisa katika halmashauri mkoani Kigoma, ziara ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, mkoani Kagera imesomba maofisa wanne mkoani humo.

Waziri Mkuu jana aliagiza Ofisa Mfawidhi wa Kituo cha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) cha Mutukula, Feisal Nassoro, na wenzake watatu warudishwe makao makuu mara moja na kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Watumishi wengine ni Gerald Mabula, George Mwakitalu na Emmanuel Malima ambao ni maofisa mapato wa TRA.

Majaliwa alitoa maagizo hayo jana wakati akizungumza na wafanyabiashara na wakazi baada ya kufanya ukaguzi kwenye Kituo cha Huduma za Pamoja Mpakani (One Stop Border Post) cha Mutukula, Missenyi mkoani Kagera.

"Watumishi hawa wanne warudishwe makao makuu kwa sababu ya kudharau mamlaka na kuikosesha serikali mapato. Ukaguzi ulifanywa na Kamati ya Usalama ya Wilaya wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya lakini walipewa dharau kana kwamba hiki ni chombo kilicho juu ya sheria.

"Mkuu wa wilaya ni mkuu na msimamizi wa shughuli za serikali ndani ya wilaya yake. Anapotaka taarifa anastahili apatiwe. Uongozi wa mkoa ulipokuja nao pia waliambulia dharau. Hatuwezi kukubali kuona mtumishi wa umma anafanya mambo ya hovyo halafu sisi tunamwacha," alisema.

"Wakati Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye ziara ya mikoa ya Kusini alisisitiza kuwa mtumishi ambaye hatekelezi majukumu yake, sisi hatutamvumilia. Ni lazima watumishi tuwe na nidhamu ya kazi, ni lazima tuheshimu mamlaka," aliwakumbusha.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu amewataka wakazi wa Mutukula wachangamkie fursa ya uwapo wao mpakani na kuimarisha biashara zao.

"Mutukula ni mji wa kibiashara na unakua kwa kasi sana. Hapa Mutukula ni sawa na Tunduma, Kasumulo, Sirari na Namanga. Lazima mji huu uwe unakimbiliwa na watu wa nje na wa ndani. Hivyo Halmashauri ya Wilaya ijipange ijenge kituo kizuri cha mabasi ili watu wakija wapate mahali pa kupumzikia," aliagiza.

Katika hatua nyingine, Majaliwa ameonyesha kukerwa na hali ya Mkoa wa Kagera kuendelea kusuasua kiuchumi kwa zaidi ya miaka kumi mfululizo licha ya kuwa na mazingira mazuri ya kiuchumi.

Kutokana na hali hiyo, ameagiza viongozi mkoani hapa kuzingatia majukumu yao katika utekelezaji wa shughuli za kimaendeleo.

Alitoa maagizo hayo juzi wakati akifunga mafunzo ya siku tano ya uongozi kwa viongozi mbalimbali wa serikali na chama mkoani hapa na kuwataka kutekeleza majukumu yao kwa vitendo ili kunusuru mkoa huo dhidi ya hali mbaya ya kiuchumi.

Majaliwa alimwagiza mkuu wa mkoa huo kuweka mikataba ya utendaji kazi na wakuu wote wa idara na vitengo katika halmashauri zote ili kukumbuka wajibu wao katika kuwatumikia zaidi wananchi na kutatua kero zao na kuwa na utaratibu wa kuwafuata, kuwasikiliza na kutafuta ufumbuzi.

Alisema tathmini ya utendaji kazi wa watumishi hao wa umma inapimwa kupitia uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwakani, ikiwa ni kipimo cha imani ya wananchi kwao.

"Simamieni kwa makini fedha zinazotolewa na serikali pamoja na za mapato ya ndani ili zitumike ipasavyo katika maeneo yenu. Miradi itekelezwe kwa ubora, ufanisi na ilingane na thamani ya fedha," alisema Majaliwa.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatma Mwassa, akisoma taarifa ya Mkoa alisema kuwa, umeshuka kiuchumi na unashika nafasi ya 25 kati ya mikoa 26.

Alisema wamefanikiwa kupanda kwa nafasi moja ambapo kwa zaidi ya miaka 10 ulikuwa ukishikilia nafasi ya 26.

Kuhusu hali ya kielimu mkoani humo, kiongozi huyo alisema ipo hatarini kutokana na namba kubwa ya wanafunzi kuacha masomo yao katika ngazi msingi na sekondari. Mwassa alisema kuwa, wamebaini kuwa wanafunzi 16,000 wa shule za msingi wameacha masomo yao huku 6,700 wa sekondari hawakumaliza kwa kipindi kilichopita.

Pia alisema mkoa huo umekumbwa na hali mbaya ya utapiamlo na udumavu kwa watu wake kwa zaidi ya asilimia 34.6.



Mratibu wa Idara ya Huduma za dharura kutoka GGML, Evarist Mwanakatwe (kushoto), akipatiwa vipimo vya saratani ya tezi dume kutoka kwa mmoja wa madaktari wa Hospitali ya Rufani ya mkoa wa Geita jana, huduma inayotolewa bure kwa ushirikiano wa GGML na hospitali hiyo katika maonyesho ya sita ya teknolojia ya madini mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama yasema hakuna sheria iliyovunjwa ukomo umri Jaji Mkuu

**Na Grace Gurisha**

WAKILI wa Kijitegemea, Humphrey Malenga, aliyefungua kesi Mahakama Kuu kupinga Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, kuongezewa muda licha ya umri wa kustaafu kufika, amegonga mwamba.

Hatua hiyo ni baada ya Mahakama Kuu ya Tanzania, Masjala Kuu, Dar es Salaam, kusema Prof. Juma kuendelea kuwepo madarakani licha ya ukomo wa umri wa kustaafu, uko sahihi kwa mujibu wa sheria.

Pia imesisitiza kuwa na pia hakuna Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyovunjwa.

Aidha, mahakama hiyo imesema imejiridhisha kuwa maombi yaliyowasilishwa na waleta maombi hayana tija kwa kuwa Jaji Mkuu ni kama majaji wengine wa Mahakama ya Rufani kwa sababu aliteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa majaji hao, hivyo uwapo wake madarakani ni kwa mujibu wa Sheria.

Jaji Godfrey Isaya, akitoa uamuzi juzi, alisema mahakama imepitia vifungu hivyo au Ibara ya Katiba, kama mleta maombi alivyoiomba mahakama ionyeshe nafasi ya Jaji Mkuu wa Tanzania. Pia imepitia mawasilisho ya pande zote mbili.

Alisema Jaji Mkuu ni mmoja wa majaji wa Mahakama ya Rufani na ili mtu apate nafasi hiyo lazima awe Jaji wa Mahakama ya Rufani na atakapokuwa Jaji Mkuu pia atabaki kuwa kama Jaji wa Mahakama ya Rufani na ataendelea kuendesha mashauri pamoja na kufanya kazi zake nyingine zitokanazo na madaraka aliyoteuliwa.

"Hivyo Jaji anaweza kuongezewa muda baada ya kustaafu au akaomba kustaafu na ukomo wake unaweza ukafika pindi atakapofariki dunia au kutenguliwa kama majaji wa Mahakama ya Rufani," alisema Jaji Isaya.

Mahakama ilifikia hatua ya kutoa ufafanuzi huo, baada ya Wakili wa Kujitegemea, Humphrey Malenga, kufungua kesi ya kikatiba kutaka mahakama hiyo itoe tafsiri ya ibara za katiba kuhusiana na ukomo wa nafasi ya jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma.

Wakili huyo alifungua kesi hiyo namba 7/2023 dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), akiomba mahakama kutoa tafsiri ya juu ya vifungu au Ibara ya 118 pamoja na Ibara ya 120 (1)(2)(3) ya Katiba, ili kuonyesha nafasi ya Jaji Mkuu wa Tanzania.

Katika kesi hiyo, Malenga alifikia hatua hiyo chini ya hati ya dharura, kutokana na taarifa zinazosambaa mitandaoni kuwa jaji huyo amestaafu tangu Juni 15,2023, lakini hadi leo bado yupo ofisini kinyume na katika ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Baada ya Malenga, kufungua kesi hiyo Juni 28, 2023 katika mahakama hiyo, jopo la mawakili wake, Ipilinga Panya, Aliko Mwamanenge na Joyce Brown, walipata hati za wito za mahakama na kuziwasilisha kwa AG.

Kesi hiyo ilitajwa Julai 3, 2023 kwa mara ya kwanza mbele ya Jaji Isaya na mawakili wa serikali, Alice Mturo na Bavoo Junus, waliomba wapewe muda ili kuwasilisha kiapo kinzani ambacho ni majibu ya kilichowasilishwa na Malenga.

Jaji Isaya aliutaka upande wa Jamhuri kuwasilisha majibu yao Julai 6, 2023 na kama kungekuwa na jambo ambalo Malenga atataka kuliwasilisha basi angefanya hivyo Julai 10, mwaka huu.

Mawakili wa pande zote mbili waliwasilisha mawasilisho yao ndipo mahakama hiyo ikafikia kutoa uamuzi huo juzi.

HABARI KITAIFA

# EWURA, LATRA zaonya upandishaji nauli

**Na Benny Kingson,** TABORA.

BAADHI ya wasafirishaji mkoani Tabora, wamedaiwa kupandisha nauli kinyemela kwa kile kinachodaiwa kuwa ni kutokana na ongezeko la bei ya mafuta ambako kwa mkoa huo lita ya petroli imepanda kwa Sh. 16.

Nauli ya Tabora Mjini kwenda Urambo imepanda kutoka Sh. 5,000 hadi Sh. 6,000, kwenda Sikonge imepanda kutoka Sh. 3,500 hadi Sh. 5,000 na bajaji imepanda kutoka Sh. 500 hadi 1,000 na kufikia Sh. 2,000.

Kutokana na upandaji huo wa kiholela, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) mkoani humo zimeonya vitendo hivyo.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake, Ofisa Mfawidhi wa LATRA Tabora, Nelson Mmari, alisema kupanda kwa bei ya mafuta siyo kugezo cha nauli kupanda kwa kuwa, kila kitu kina utaratibu wake.

Mmari alisema kuwa hakuna ongezeko la nauli lililotangazwa mpaka sasa na wao ndiyo wenye dhamana hiyo ya kutangaza.

"Abiria mtakaopandishiwa nauli mtoe taarifa LATRA kupitia namba ya simu ya bure 0800110019, mhakikishe mnakata tiketi kielektroniki kwa basi ziendazo mikoani na za kawaida kwa wasafiri wa ndani,"alisema Mmari.

Ofisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala EWURA Mkoa wa Tabora, Sakina Yusufu, aliwahimiza wadau na wananchi kuwa na tabia ya kupata taarifa sahihi kuhusu gharama halali za tozo ya maji na mafuta kutoka katika mamlaka husika.

"Wadau na wanachi hususani wasafiri watambue kuwa ongezeko la bei ya mafuta lililotangazwa na serikali kupitia EWURA halitoi mwanya wa nauli kupanda ama kupandisha nauli kiholela . Hili ni kosa kisheria hivyo mtoe taarifa kwetu kupitia namba 0746478361 ili tuchukue hatua haraka," alisema.



Shekhe wa Wilaya ya Ilala, Adam Mwinyipingu (wa tatu kushoto), akikabidhi msaada wa maji na vitu mbalimbali vilivyotolewa na ofisiya Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA) Ilala kwa Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya J.A.I, Bin Daud inayojihusisha na kutoa huduma katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Amana, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Biteko ataka utatuzi wa kero za wananchi vijijini

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

NAIBU Waziri Mkuu, Dotto Biteko, amewataka viongozi kutoa kipaumbele kwa wananchi ambao wanaishi vijijini kwa kuwapa huduma zote muhimu ili kupunguza kero ambazo zimekuwa zikiwakabili.

Biteko alitoa kauli hiyo jana wilayani Sengerema mkoani Mwanza akiwa safarini kuelekea mkoani Geita katika uzinduzi wa maonyesho ya kimataifa ya Madini na kuwaagiza viongozi kuhakikisha wanatoa huduma vijijini ili kuondoa kadhia ya wananchi kwenda mjini kuzitafuta.

Kiongozi huyo ameahidi kupeleka matatizo yote ya wilaya hiyo kwa Rais Samia Suluhu Hassan ili yafanyiwe kazi.

Biteko alisema tangu aachanguliwe na hajawahi kushukuru hivyo kwa kuwa hicho ni kikao chake cha kwanza na wananchi, amemshukuru (Rais) kwa kumwamini na kumchangua.

Mbunge wa Sengerema, Khamis Tabasamu, aliiomba serikali kupeleka vifaa tiba kwenye Hospitali ya Wilaya iliyoko Mwabaruhi ili itakapokamika ifunguliwe ikiwa na vifaa vyote vya kutolea huduma.

Mbunge huyo aliiomba serikali kuwatengenezea barabara iliyoaidiwa na Rais wa Awamu ya Tano, John Pombe Magufuli yenye urefu wa kilometa 15.

# Tume sheria yakabidhi ripoti kwa Waziri wa Katiba na Sheria

**Na Thobias Mwanakatwe,** DODOMA

TUME ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT) imewasilisha ripoti mbili za mapitio ya mfumo wa sheria unaosimamia makosa dhidi ya maadili na taarifa ya mapitio ya mfumo wa sheria unaosimamia udhamini nchini baada ya kufanyiwa utafiti.

Ripoti hizo zilikabidhiwa jana kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Pindi Chana, baada ya kufanya ziara katika ofisi ya tume hiyo na kukutana na watumishi mjini hapa.

Akizungumza kabla ya kukabidhi taarifa hiyo, Mwenyekiti wa tume hiyo, Jaji (mstaafu) January Msofe, alisema katika kukamilisha mapitio ya sheria zinazohusu makosa dhidi ya maadili, tume ilikusanya maoni ya wadau katika mikoa 18.

Alitaja mikoa hiyo kuwa ni Dodoma, Singida, Mwanza, Mara, Dar es Salaam, Katavi, Geita, Shinyanga, Pwani, Tanga, Iringa, Mbeya, Arusha, Manyara, Mtwara, Lindi, Tabora, Ruvuma na Kigoma.

Jaji Msofe alisema walihojiwa ni pamoja na majaji, mahakimu, waendesha mashtaka, mawakili wa kujitegemea, wapelelezi, maofisa ustawi wa jamii, viongozi wa dini, walimu wa shule za msingi na sekondari, watendaji wa mitaa na asasi za kiraia zinazotoa msaada wa kisheria.

Jaji Msofe alisema utafiti kuhusu makosa dhidi ya maadili ulibainisha yanaongezeka siku hadi siku na kuwa tishio kwa taifa .

"Katika mwaka wa 2021 makosa 7,601 ya kubaka na kulawiti yaliripotiwa na mwaka 2022 makosa 8,413 yaliripotiwa, hata hivyo, kesi zinazofunguliwa mahakamani ni chache kuliko zile zinazotolewa taarifa katika vituo vya polisi, " alisema.

Alitoa mfano katika kipindi cha 2021/22 na 2022/23 kuwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilifungua mahakamani kesi 2,980, na 4,294 za makosa dhidi ya maadili yakiwemo ya ukatili, kubaka, kujaribu kubaka, kulawiti na kujaribu kulawiti.

Mwenyekiti huyo alisema kwa mujibu wa utafiti, kuna idadi kubwa ya kesi za makosa ya dhidi maadili ambayo hayajaripotiwa katika vyombo husika.

Alibainisha kuwa makosa dhidi ya maadili yanayotokea mara kwa mara katika jamii ni ubakaji; ulawiti; utoroshaji wa watoto wa kike wenye umri chini ya miaka 16 na shambulio la aibu.

Kuhusu taarifa ya mfumo wa sheria unaosimamia udhamini, alisema utafiti umebaini baadhi ya watuhumiwa wa makosa dhidi ya maadili huruka dhamana hususan waliopo mikoa ya mipakani na kushiriki kuharibu ushahidi kwa kuwatisha mashahidi na kurudia makosa waliyoshtakiwa nayo.

Jaji Msofe alisema utafiti huo umebainisha changamoto mbalimbali zikiwamo malalamiko kuhusu watoto kuchanganywa na watu wazima gerezani, hivyo kujifunza mbinu za uhalifu na kuhatarisha maisha yao.

Nyingine ni mahakama za watoto kukosa miundombinu rafiki kwa ajili ya kusikiliza kesi na uhaba wa maofisa ustawi wa jamii unaosababisha mashauri kuchelewa kutolewa hukumu mahakamani.

Waziri Chana aliipongeza tume hiyo kwa jitihada wanazozifanya kupitia sheria na kuja na mapendekezo ambayo utekelezaji wake unaipa Tanzania heshima ndani na nje ya nchi.

Alisema utafit uliofanyika kuhusu sheria zinazosimamia maadili zitakuwa chachu kuimarisha utamaduni. Mila, desturina kukuza uhusiano baina ya mataifa.

Pia alizipongeza taasisi za dini kwa kuimarisha maadili ya Watanzania na kuahidi kuendelea kushirikiana nazo kudumisha amani nchini.

"Naipongeza sana Tume ya Kurekeibisha Sheria kwa namna wanavyojitahdi kutafiti sheria na kuja na mapendekezo muhimu, mapendekezo mnayotuletea yamekuwa chanzo cha utulivu wa taifa na zimesisimua ukuaji wa uchumi nchini," alisema.

Awali, akimkaribisha Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Griffin Mwakapeje, alisema tume imeandaa ripoti 56 kuhusiana na sheria mbalimbali nchini huku akibainisha taasisi hiyo imekuwa ikishirikiana nyingine za ndani na nje ya nchi kufanikisha majukumu kwa ufanisi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ziara za Rais, Waziri Mkuu ziwaamshe viongozi mikoani

**WIKI** iliyopita na mapema wiki hii, Rais Samia Suluhu Hassan alifanya ziara ya kikazi katika mikoa ya Mtwara na Lindi kwa ajili ya kufanya uzinduzi na kukagua miradi ya maendeleo pamoja na kuzungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara.

Katika ziara hiyo, Rais aliongozana na mawaziri wanaoshughulikia masuala mbalimbali kama vile ujenzi, kilimo, mifugo na uvuvi, uchukuzi na serikali za mitaa ambayo yanawahusu wananchi moja kwa moja. Mbali na Rais Samia, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alifanya ziara wiki hii mkoani Kigoma na sasa anaendelea mkoani Kagera.

Akiwa mkoani Mtwara, Rais Samia alibaini madudu yanayofanywa na viongozi na watendaji katika ngazi za wilaya hasa kwenye halmashauri, yakiwamo ya ubadhirifu wa mamilioni ya shilingi zilizopelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Moja ya madudu hayo ni ubadhirifu wa fedha za ruzuku ya mbolea ambazo hutolewa na serikali kwa ajili ya kupunguza makali ya bei hiyo kwa wakulima ili wazalishe kwa wingi.

Kutokana na kuwapo kasoro kama hizo katika usimamizi wa fedha na kukwamisha miradi mingi ya maendeleo, Rais Samia alihoji kama katika maeneo hayo kuna viongozi wanaotakiwa kusimamia. Pia alishangaa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kujikita katika kupambana badala ya kuzuia kwa kufanya uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu pekee.

Baada ya kujionea hayo yote, Rais jana alitangaza mabadiliko ya baadhi ya watendaji ambayo kwa kiasi kikubwa yamegusa mkoa wa Mtwara kwa kutengua katibu tawala wa mkoa, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya na wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa. Ni dhahiri kwamba mabadiliko hayo katika mkoa huo, yamechagizwa na kasoro hizo zilizobainika katika ziara ya Rais.

Katika mkoa wa Kigoma pia, Waziri Mkuu alikutana na kasoro mbalimbali zikiwamo za ubadhirifu wa fedha zikiwamo za ujenzi wa miundombinu ya hospitali ya wilaya ya Uvinza hatua ambayo ilimlazimu kuagiza mkurugenzi wa halmashauri na mweka hazina kusimamishwa mara moja. Sambamba na maofisa hao kusimamishwa, Majaliwa pia aliagiza timu kutumwa kwenda kufanya uchunguzi wa upotevu wa fedha katika miradi kadhaa ya maendeleo.


Yaliyoibuliwa na Rais na Waziri Mkuu ni mifano juu ya mambo yanayotendeka kwenye mamlaka za serikali za mitaa kwa watendaji kujichotea fedha za miradi ya maendeleo kwa lengo la kuwaondolea wananchi kero zao. Kama alivyosema Rais Samia, inashangaza kuona kuwa wako wakuu wa mikoa, wilaya na makatibu tawala lakini wanashindwa kufuatilia na kuchukua hatua dhidi ya watuhumiwa wa ubadhirifu mpaka viongozi watakapofanya ziara.

Katika halmashauri kuna madiwani ambao ndio jicho la serikali katika kuwasimamia watendaji huku wakuu wa mikoa, wilaya na makatibu tawala wakiwa ndio wasimamizi wa mali za serikali. Je, ni kwa nini mambo hayo yanatokea na hakuna hatua zinazochukuliwa? Madiwani nao ni sehemu ya kunufaika na fedha hizo na kukwamisha shughuli za maendeleo?

Kuwapo kwa hali hiyo, kunadhihirisha kwamba kuna ulegevu mkubwa katika usimamizi wa mali na rasilimali za serikali katika ngazi za halmashauri. Hali hiyo inatokana na viongozi waliopewa dhamana kutowajibika na kuwa katika usingizi wa pono. Haiwezekani mambo yaende hovyo ilhali kuna viongozi waliopewa dhamana huku mambo yakiendelea kuharibika.

Ni vyema ziara iliyofanywa na Rais Samia mkoani Mtwara na ile ya Waziri Mkuu mkoani Kagera, ziwaamshe kutoka usingizini viongozi waliopewa dhamana katika mikoa na wilaya. Vinginevyo wananchi wataendelea kushuhudia Rais akifanya pangua pangua na kutengua uteuzi kila uchao huku miradi ya maendeleo ikiendelea kudorora.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Imani potofu isipewe nafasi kampeni ya chanjo ya polio

**KAMPENI** ya chanjo dhidi ya ugonjwa wa polio kwa watoto milioni 3.2 walio chini ya umri wa miaka nane, iliyoanza Septemba 21 inatarajiwa kuhitimishwa leo.

Kampeni ilifanyika katika mikoa ya Rukwa, Kagera, Kigoma, Katavi, Songwe na Mbeya, baada ya mtoto mmoja mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi 11 kupata ugonjwa huo Mei mwaka huu, katika Manispaa ya Sumbawanga, mkoani Rukwa, ndipo serikali ikaamua kuchua hatua hiyo ili kuudhibiti.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema mbele ya waandishi wa habari jijini Dodoma hivi karibuni kwamba watashirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na wadau wa sekta ya afya kuendesha kampeni ya chanjo katika mikoa hiyo.

Pamoja na kwamba kampeni inahitimishwa leo, ninadhani bado kuna haja ya kukumbusha wazazi na walezi kuhakikisha watoto wao wanapata chanjo, ili wawe kinga dhidi ya ugonjwa huo hatari unaoelezwa kuwa unaweza kusababisha ulemavu au kifo.

Ninaeleza hivyo, kwa sababuutoaji wa chanjo hiyo huwa unakumbwa na changamoto katika baadhi ya maeneo, huku baadhi ya wazazi na walezi wakiamini kwamba zina madhara au hoja nyingine zisizo na mashiko.

Siamini kwamba serikali inaweza kuleta vitu ambavyo ni hatari kwa wananchi wake, hivyo ni vyema kutambua kuwa hiyo ni fursa nzuri kwao kuhakikisha watoto wao wanachanjwa.

Imani potofu dhidi ya chanjo hiyo na hata za magonjwa mengine, isingefaa kupewa nafasi, kwani inaweza kusababisha baadhi ya watoto wasichanjwe, hali ambayo inaweza kuwafanya wawe katika hatari ya kukumbwa na ugonjwa huo hatari.

Katika baadhi ya maeneo, wapo watu wanaoamini kuwa kumchanja mtoto kinga ya ugonjwa wa polio ni kumsababishia ugumba wakati wa utu uzima, jambo ambalo sidhani kama lina ukweli ndani yake.

Ummy ameshaweka wazi kuwa maambukizi ya virusi vinavyosababisha ugonjwa huo, yametolewa taarifa pia katika nchi zinazopakana na Tanzania, ikiwamo Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Zambia.

Katika ufafanuzi wake, ni kwamba hali hiyo inaongeza tishio na hatari ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo kwa Tanzania hasa katika mikoa inayopakana moja kwa moja na nchi hizo.

Waswahili wana msemo wao kwamba; 'ukiona mwenzio ananyolewa, na wewe zako tia maji', hivyo kwa taarifa hiyo ni wazi kuna haja ya kuchukua tahadhari kama ambavyo serikali imeamua kufanya.

Yako mambo muhimu ambayo jamii inapaswa kuyazingatia siku zote hata kama hakuna kampeni. Mojawapo ni usafi, kwani inaelezwa kuwa uchafu unachangia kueneza ugonjwa huo.

Wataalam wa afya wanaeleza kuwa ugonjwa huo husababishwa na kirusi cha polio, kinachoenezwa kwa kula chakula na kunywa maji yaliyochafuliwa na kinyesi cha mtu aliyeambukizwa ugonjwa huo.

Katika ufafanuzi wao ni kwamba ugonjwa unaweza kumpata mtu kwa kutozingatia kanuni za usafi, na iwapo mtoto mmoja atapata maambukizi, watoto wote watakuwa kwenye hatari ya kuambikizwa polio.

Vilevile, polio hushambulia mishipa ya fahamu na kusababisha kupooza kwa misuli hasa miguu au mikono yote kwa pamoja, na wakati mwingine misuli ya kifua inayosaidia kupumua na kusababisha kifo.

Dalili za ugonjwa huo zinatajwa kuwa ni pamoja na mgonjwa kuwa na homa kali, mafua, maumivu ya mwili, maumivu ya kichwa na shingo, ulemavu wa ghafla wa viungo.

Watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, wanatajwa kuwa kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa ugonjwa huo, ingawa pia inaelezwa kwamba unaweza kuwapata watu wa rika zote.

Ni vyema kuokoa maisha ya watoto kwa kuwapa chanjo, si kuegemea kwenye imani na kusababisha madhara kwao. Ni muhimu wazazi na walezi kulinda afya za watoto bila kuingiza imani potofu.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Ukipewa hadhi iheshimu ili ikustahilishe



Pascal Mayalla

SEPTEMBA Mosi, mwaka huu, ilitolewa taarifa ya Ikulu kuhusu aliyekuwa Balozi Dk. Willibrod Slaa, kufutiwa hadhi ya ubalozi. Taarifa hiyo ya Ikulu haikutoa sababu za kumfutia hadhi hiyo.

Hatua hii imezua mjadala mkubwa kwenye mitandao ya kijamii, wengi wakijaribu kuelezea sababu za kufutiwa hadhi ya ubalozi kuwa ni ukosoaji wake wa mkataba wa uendeshaji wa babdari zetu kati ya serikali na kampuni ya DP World kutoka Dubai.

Kwanza naomba ifahamike wazi, hakuna kosa lolote kwa mtu yeyote, mwenye hadhi yoyote, kufanya ukosoaji wowote wa jambo lolote ilimradi ukosoaji huo haukiuki sheria yoyote.

Kwa hiyo, Dk. Slaa ana haki ya kukosoa jambo lolote kama ilivyotolewa na ibara ya 18 ya Katiba yetu kwenye uhuru wa kutoa maoni na uhuru wa kujieleza.

Ubalozi ni hadhi ya kimataifa inayoendana na haki na marupurupu fulani zikiandamana na kinga, hivyo ubalozi una masharti ya kufuatwa mtu unapokuwa Balozi kuna vitu hutakiwi kuvifanya.

Miongoni mwa haki na kinga ya kibalozi ni pamoja na kutokushitakiwa popote kwa kosa la jinai. Mtu yeyote mwenye hadhi ya ubalozi akitenda jinai yoyote, kabla hajapandishwa mahakamani kushitakiwa, hatua ya kwanza ni kuvuliwa kwanza hadhi ya ubalozi, ndipo ashitakiwe.

Hii si mara ya kwanza kwa mtu mwenye hadhi ya ubalozi kuvuliwa hadhi hiyo. Wa kwanza alikuwa Balozi wa Kwanza nchini Uingereza, Christopher Kasanga Tumbo.

Alivuliwa ubalozi na kushitakiwa kwa jinai enzi za awamu ya kwanza ya utawala wa nchi chini ya Mwalimu Julius Nyerere. Mwingine ni Balozi Antony Ngaiza aliyevuliwa ubalozi na kushitakiwa kwenye kesi ya uhaini ya mwaka 1982.

Pia Balozi Prof. Costa Rick Mahalu alivuliwa hadhi ya ubalozi na kushitakiwa kwa uhujumu uchumi ununuzi wa jengo la ubalozi wa Tanzania, Rome nchini Italia.

Aliposhinda kesi na kukutwa hana hatia, alirejeshewa ubalozi wake. Kwa hiyo hata kwa Dk. Slaa tusubiri yatokanayo na kufutiwa hadhi ya ubalozi, yakishindwa kuthibitishwa, anarejeshewa ubalozi wake.

Kwa vile hili ni andiko elimishi, nichukue nafasi hii kuelimisha mambo kadhaa. Baadhi ya mambo hayo ni hadhi ya ubalozi ni nini?; Sifa za mtu kuwa na hadhi ya ubalozi ni zipi; kuna cheo cha ubalozi na Ubalozi wa kuteuliwa?; Zipi ni haki na hadhi ya kidiplomasia; kinga ya ubalozi; kila balozi lazima awakilishe nchi?; je, maofisa wote ubalozini ni mabalozi au wana hadhi za ubalozi?; makosa gani yanampotezea mtu hadhi ya ubalozi?; kila mwanadiplomasia anayefanya jinai ni lazima avuliwe Ubalozi?.

Kama nilivyoeleza awali, Balozi maana yake ni mwakilishi au mjumbe.

Hata Balozi wa nyumba 10 ni mwakilishi wa nyumba 10 mtaani.

Enzi za chama kimoja, mabalozi wa nyumba 10 walikuwa na nguvu kubwa sana. Kitaifa, balozi ni mwakilishi wa nchi moja kwenye nchi nyingine.

Hadhi ya ubalozi ni heshima anayokuwa nayo huyo mwakilishi, hadhi inayoitwa 'diplomatic status'. Mtu mwenye hadhi ya ubalozi anakuwa na heshima inayoambatana na baadhi ya haki na kinga.

Hadhi kubwa ya kwanza ni kupatiwa paspoti ya kibalozi (diplomatic passport), hivyo anakuwa katika kundi la watu maalum (VIP). Akisafiri anapitia sehemu ya watu maalumu na kupatiwa huduma zinazoitwa za kidiplomasia.

Haki na kinga hizo za kibalozi zinaongozwa na mkataba wa kimataifa wa Vienna Convention kuhusu uhusiano wa kidiplomasia. Kila nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) lazima iuridhie, hivyo Tanzania tumeridhia. Mkataba wa Vienna uliridhiwa Aprili 14, 1961 hivyo Tanzania tumeingizwa na wakoloni tulipokuwa bado Tanganyika. Hata hivyo Bunge la Tanganyika liliridhia Juni 24, 1964 na aliyekuwa Balozi wa Tanzania katika Umoja wa mataifa, Chief Erasto Mang'enya akaziwasilisha katika masijala kuu ya UN kwa NV Na. 7311.

**SIFA NA HADHI YA UBALOZI**

Mtu yeyote mwenye elimu yoyote na sifa zozote anaweza kuteuliwa kuwa Balozi, hakuna kigezo cha elimu wala uzoefu, ila maofisa ubalozi ndio wanapaswa kuwa na sifa fulani fulani. Kabla ofisa ubalozi yoyote hajapatiwa kituo cha kazi, wasifu wake na taarifa kuhusu maisha yake kwa ujumla hutumwa nchi husika.

Baada ya hapo, nchi husika inawatumia maofisa wake kwa ajili ya kuthibitisha taarifa hizo kabla ya kuruhusiwa kwenda huko. Mtu huyo akishawasili huko, hufanyiwa 'security clearance', ndipo nchi husika imruhusu balozi kupeleka hati za utambulisho kwa mkuu wa nchi husika.

Hapa nchini, kuna mabalozi wamewahi kukataliwa kuziwakilisha nchi zao wakiwamo kutoka nchi za Ulaya hususan zile zenye tabia za ajabu ajabu ambazo nchini mwetu hazikubaliki.

Pia kuna balozi wetu mmoja baada ya kukubaliwa, alipofika nchi husika, utambulisho wake uligomewa kupokewa kwa muda mrefu lakini baadaye akakubaliwa. Hivi karibuni alipokula uteuzi fulani mnene, ndipo ilijulikana kwa nini nchi ile ilitaka kumgomea.

Ifahamike kwamba kuna cheo cha ubalozi (career diplomat) na ubalozi wa kuteuliwa. Kuna mabalozi ambao ni wanadiplomasia kitaaluma. Kwa mfano katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, mtu anapanda cheo hadi kufikia ngazi ya juu kabisa ya balozi.

Pia kuna mabalozi wa kuteuliwa tu. Hawa wakiboronga ndio hadhi yao ya ubalozi inafutwa. Lakini wale wanadiplomasia kitaaluma (carrier diplomats) ubalozi wao ni cheo, hawezi kufutwa ila anaondolewa hadhi na bado anaendelea kuwa balozi. Mabalozi wana diplomasia wakivuliwa hadhi ya ubalozi, baadaye utajua sababu, lakini wale wengine wakivuliwa hadhi ya ubalozi, itatangazwa tu lakini sababu hazielezwi.

Tutaendelea wiki ijayo

**Wasalaam**

**Paskali**

**0754 270 403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tuache uheshimiwa turejeshe udugu tukwamuke



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

NIKIKAA pembeni nikimwangalia Chifu Hangaya, namwona anavyohangaika na watu wake. Anahangaikia maisha ya Watanzania wa kila rika, kila rangi na maumbile.

Lakini namwona akihangaishwa na waheshimiwa wake, waheshimiwa kama yeye, waheshimiwa aliowateua yeye na wengine ni waheshimiwa tuliowachagua sisi.

Kila anakokwenda nchi hii, Chifu Hangaya analiliwa na wananchi. Unajiuliza ni kwa nini mpaka aende yeye ndipo wananchi waibuke na kumlalamikia, wengine wakiwa na mabango?

Inamwuma pale anapojikuta anashuhudia au kusikia kuwapo watu wa chama chake, Chama Cha Mapinduzi (CCM) mahali fulani, wameamua kubwaga manyanga uanachama na kumrudishia kadi za chama chao.

Inamkera kwa kuwa yeye ndiye kinara anayetakiwa kuhakikisha wanachama wanaongezeka na si kupungua, kwa sababu tu kuna mashetani fulani hawataki kutenda sahihi.

Anajikuta siku nyingine hapepesi macho na kuwatengua katika nafasi zao na kuweka wengine, lakini anapokosea ni kuwapeleka kwingine. Mtu akiharibu mahali, akae pembeni atazame wengine wanafanya nini.

Mimi na akili zangu hizi huwa sikubaliani kabisa na mharibifu kupewa kwingine akaharibu na kusababisha malalamiko yale yale! Tunajionea hivi sasa miaka zaidi ya 60 ya uhuru, maji na umeme ni vya kutafuta. Leo!

Hiyo ni kutokana na watu kupewa majukumu na dhamana na badala yake wanaharibu, baada ya kuhakikisha kuwa matumbo yao yako salama, wanaomba bora waharibu, kwani watahamishiwa kwingine kufanya hayohayo.

Sitaki kumpangia Chifu Hangaya nini cha kufanya lakini nadhani angeliangalia hilo kwa sababu Watanzania hivi sasa tuko milioni 62 na ushei na tupo wenye nia njema na nchi hii na wapo wanaotazama zaidi 'Tumbo Street'.

Hata tukiangalia historia ya nchi hii, tutaona kuna watu wamo serikalini miaka nenda rudi, lakini hawana tija yoyote. Kuna watu tangu serikali ya awamu ya nne, wamo kwenye Baraza la Mawaziri lakini hatuoni tija. Wapo (kwa sauti ya Makongoro)!

Waondoke hao wabaki wenye tija ou mapengo yazibwe na wenye tija, wapo watu wenye ubunifu wanaoweza kumsaidia Chifu Hangaya kutuliza kilio cha wanakondoo wake, lakini tatizo ni fursa.

Baadaye siku zijazo nitapendekeza kwenye Katiba mpya, mawaziri wasitokane na wabunge, kwa sababu uzio ule unatulazimisha kuteua watu ambao wengine hawana tija bali umaarufu tu wa kisiasa.

Kwa hali hiyo, tunajikuta tumeacha nje wanaoweza kutusaidia, huku zizini tukibaki na wachumia tumbo, wanaodhani nchi hii ni yao peke yao na wamezaliwa kuvuna, kula na kusaza wengine tukilia njaa.

Lingine nadhani ni hili la kuitana 'mheshimiwa'. Enzi za Mwalimu Julius Nyerere, aliondoa ubaguzi huo wengine kuonekana wa maana katika jamii na wengine 'viatu' wasio na faida, akapendelea tuitane ndugu.

Tuliitana ndugu kuanzia Ndugu Rais, Ndugu Makamu wa Rais, Ndugu Waziri Mkuu, Ndugu Waziri, Ndugu Naibu Waziri, Ndugu Spika, Ndugu Mbunge, Ndugu Mkuu wa Mkoa, Ndugu Mkuu wa Wilaya, Ndugu Diwani, Ndugu Jaji, Ndugu Hakimu.

Heshima ikaendelea kutamalaki licha ya nafasi tulizokuwa nazo. Sote tukaonekana sawa, viongozi wakitenda haki na kuona wako sawa na wasio na nafasi serikalini au katika taasisi.

Baada ya Mwalimu Nyerere kutangulia mbele za haki, wale waliokuwa mstari wa mbele kuhanikiza kuwa tutamuenzi, ndio haraka haraka wakaja na pepo mbaya wa kujiaminisha kuwa kiongozi ni Mungumtu na wananchi ni vidampa tu.

Wakaja na Mheshimiwa Rais mpaka Mheshimiwa Diwani na Mheshimiwa Hakimu. Likaibuka pengo la ubaguzi kwamba wewe kama huna nafasi ni marufuku kuitwa mheshimiwa, utabaki kwenye kundi la 'mabibi na mabwana'.

Ubaguzi huo ndio umefanya hata sasa wananchi wasihudumiwe kikamilifu. Ubaguzi huo ukafanya baadhi ya wakuu wa wilaya na mikoa kwa kuitwa tu waheshimiwa, wakajipa madaraka ya kupora na kudhulumu mabibi na mabwana kwa kaulimbiu ya 'maagizo kutoka juu'.

Pengo la heshima lililopo kati ya kiongozi na mwananchi wa kawaida, ni kikwazo katika kuleta maendeleo katika nchi hii, kwa sababu sasa mabibi na mabwana wanajiona si shemu ya nchi, bali ni watwana tu huku waheshimiwa wakijiona ni wenye nchi na ni mabwana.

Kama tutaendelea na hali hii ya watu kulazimisha uheshimiwa na kuwaona wananchi ni watu wa chini wasiostahili heshima, hakika tutaendelea kukwama kwenye tope la maendeleo.

Hakika wananachi wataiacha nchi kwa waheshimiwa na kila mtu kuamnbania hali yake, lakini tukirejea kuonana ndugu na kuitana ndugu, bila shaka nchi itakuwa yetu na tutaijenga pamoja kama ndugu.

Tuheshimiane katika maendeleo lakini tusiheshimiane katika kunyanyasana na kuona wengine wanastahili na wengine hawastahili, lakini kubwa tupeane nafasi kwa uwezo na si umaarufu ili tusonge mbele. Tumwombee Chifu Hangaya atuvushe. **Amina!**

# Karakana kimataifa uchomeleaji vyuma kujengwa D'Salaam

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Ufundi Don Bosco cha Oysterbay, Dar es Salaam, kinatarajia kujenga karakana ya kimataifa itakayotoa mafunzo ya uchomeleaji vyuma kwenye miradi mikubwa ya ujenzi na viwandani.

Karakana hiyo itakayojengwa kwa ufadhili wa taasisi ya kimataifa ya GFP ya Marekani itakuwa na vifaa vya kisasa na ya kwanza Afrika Mashariki kwa ubora.

Uzinduzi wa ujenzi huo ulifanyika jana kwenye chuo hicho na kuhudhuriwa na viongozi wa taasisi hiyo, akiwemo Mwanzilishi wa GFP, Michael Vallez.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo, Mwakilishi Mkazi wa GFP, Hilu Bura, alisema lengo la taasisi hiyo ni kujenga karakana yenye hadhi ya kimataifa ili wanafunzi watakaomaliza kwenye chuo hicho waweze kupata vyeti vya kimataifa.

Alisema wahitimu watakaopata mafunzo kwenye karakana hiyo, watakuwa na uwezo wa kupata kazi ndani na nje ya nchi kwani watakuwa wakitambulika.

Hilu alisema lengo la kujenga karakana hiyo ni kutaka kufikia viwango vya kimataifa na kuwataka wanafunzi watakaopata fursa ya kupata mafunzo hayo kuyatumia kikamilifu.

"Mnapokuwa hapa chuoni msifikirie mambo madogo madogo kwa sababu mnatakiwa kufanya mambo makubwa ambayo hata dunia itaona na kujifunza, kwa hiyo lazima tubadili tunavyofikiri,"

"Napenda niwaambie wanafunzi kwamba hakikisha unatimiza ndoto yako na mnapokuwa na walimu wenu msiogope kuuliza mnapokuwa na maswali sehemu ambapo hamjaelewa," alisema Hilu

Alisema amekuwa kwenye sekta ya mafuta kwa zaidi ya miaka 12 akisimamia meli zinazokuja nchini kwa ajili ya kukamilisha taratibu zinazohitajika.

Aliwataka wasichana kuchangamkia fursa za masomo ya uchomeleaji vyuma na kuachana na dhana kwamba fani hiyo ni kwa ajili ya wanaume pekee.

"Wasichana lazima mbadilike na mfikiri tofauti kuhusu fani hii ya uchomeleaji vyuma kwa sababu kuna miradi mikubwa inayohitaji wataalamu wa kimataifa lazima msomee fani hii ili muweze kushiriki kwenye ujenzi wa miradi hii, " alisema Hilu.

Mwanzilishi wa GFP, Michael Vallez, alisema miaka 30 iliyopita alipokuwa akitembelea mataifa mbalimbali duniani alipata ndoto ya kusaidia vijana kwa kuwapa elimu ya ufundi na sasa anaona inaanza kutimia.

"GFP imeweza kutoa elimu ya ujuzi kwa vijana wa mataifa mbalimbali ikiwemo Tanzania na kwa kweli najivunia kuona ndoto yangu inatimia na nitaendelea kusaidia vijana wengi ili wapate ujuzi utakaowasaidia kupata ajira," alisema

Alisema lengo la taasisi yake ni kutoa mafunzo kwa nguvu kazi ya viwandani kwa nchi nyingi za Afrika na kufikia viwango vya kimataifa kupitia vyuo vya ufundi, serikali na viwanda.

"Tunalenga kuboresha mafunzo ya nguvu kazi ya viwandani kwa maelfu ya vijana na lengo hasa ni kupata watu 5,000 watakaokuwa na ujuzi wa uchomeleaji vyuma wenye vyeti vya kimataifa ambao wanaweza kufanyakazi kokote duniani ifikapo mwaka 2027," alisema Vallez

Mwalimu wa chuo hicho, Erick Nkula, alisema karakana hiyo itatoa mafunzo ya kimataifa yenye vifaa vya teknolojia ya hali ya juu ili kuwezesha vijana watakaohitimu kutambulika kimataifa.

Alisema karakana hiyo inatarajiwa kuanza kujengwa Novemba mwaka huu na baada ya kukamilika watapata wanafunzi kutoka nje ya nchi.

# Silaa amaliza mgogoro Bwawa la Mindu

**Na Munir Shemweta,**
MOROGORO

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amehitimisha mgogoro wa ardhi katika hifadhi ya bwawa la Mindu, mkoani hapa huku akibainisha kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza wananchi 357 waliovamia eneo hilo mita 500, kupatiwa viwanja.

Uamuzi huo unatokana na mgogoro wa muda mrefu baina ya wananchi na serikali kutokana na uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975, kutaka wananchi hao kuondolewa ili kulinda chanzo hicho cha maji.

Akizungumza na wananchi hao juzi wakati akifuatilia utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri, Silaa alisema madai ya wananchi kuwa umbali wa mita 500 ulioanishwa kulinda eneo la bwawa la Mindu hayana ukweli kwa kuwa lengo la serikali si kujipatia eneo bali kulinda chanzo hicho cha maji.

''Ingelikuwa tunapima halafu tunawaondosha wananchi na kugawana viwanja, kimoja RC (mkuu wa mkoa), kingine DC (mkuu wa wilaya) na kamishna tungesema tunawabana ili tupate maeneo.

Tunapima kulinda bwawa ambalo mimi si mkazi wa eneo hili. Tunalinda bwawa hili kwa faida wa wana Morogoro mkiwemo ninyi," alisema.

Kuhusu uthamini uliofanyika, Silaa alisema hiyo ilikuwa kazi maalumu ambayo ilibaini wananchi walioko ndani ya mita 500 kuwa wako kwenye eneo la hifadhi la bwawa la Mindu na kubainisha kwamba ndipo linapokuja suala la haki halali na ile haramu.

''Fidia ya hapa si iliyotokana na mtu aliyechukuliwa ardhi yake yenye mali ndani yake bali ni fidia iliyotokana na busara, hekima na huruma ya Rais. Tungelifuata uamuzi wa Baraza la Mawaziri wa Septemba 23, 2019 maana yake mkuu wa wilaya angeagizwa kufikia tarehe fulani kila mtu aondoke,'' alisema Silaa.

Kwa mujibu wa Waziri Silaa, fidia kwa wananchi waliovamia eneo la hifadhi ya bwawa la Mindu haipo lakini kwa mujibu wa wataalamu wa ardhi, wananchi 357 ndio wanaopaswa kulipwa kifuta jacho ikiwa ni huruma ya Rais Samia Suluhu Hassan kama mkono wa heri kuwasaidia kuhamisha mali zao.

Alisema baada ya kufanya mawasiliano na Rais Samia, alimwelekeza amwambie Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Morogoro awapatie viwanja wananchi wanaopisha uhifadhi wa eneo la bwawa ili kujenga nyumba za kuishi.

Awali, Diwani wa Mindu, Zuberi Mkalaboko, alimweleza Waziri Silaa kuwa wananchi wa eneo hilo hawana tatizo la kupisha uhifadhi wa bwawa isipokuwa kero zao kubwa ni tatu ambazo alizitaja kuwa ni ushirikishwaji, vipimo vilivyofanywa na wataalamu wa ardhi na fidia wanayotaka kulipwa.

Waziri Silaa mbali na kutembelea eneo la Mindu na CCT- Forest, alihitimisha ziara yake ya siku moja mkoani Morogoro kwa kutembelea kata ya Chamwino eneo lenye mgogoro la Pombe Shop ambako ilimlazimu kuutatua mgogoro wa eneo hilo usiku.

Katika kuhitimisha mgogoro huo, alimwelekeza Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Morogoro kuwatafutia viwanja wananchi 57 kuondoka kwa hiari kupisha ujenzi wa shule.

''Tumekaa hapa mpaka usiku kuhangaikia watoto wenu, eneo hili lilikuwa la umma na litaendelea kuwa la umma','' alisema Silaa.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa (kulia), akiangalia moja ya nyaraka za mwananchi alipotembelea ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoa wa Morogoro akiwa katika ziara yake mkoani humo juzi. **PICHA: WIZARA YA ARDHI**

# Mhitimu NIT asifu shahada ilivyomsaidia ufanisi wa kazi

**Na Mwandishi Wetu**

MHITIMU wa shahada ya usimamizi wa biashara ya Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Joachim Kimaro (pichani), amesifu ubora wa kozi hiyo ambayo imemwezesha kufanya kazi kwa ufanisi katika Benki ya CRDB.

Shahada hiyo ni moja ya kozi maarufu kwa wanafunzi wanaotamani mafanikio makubwa katika usimamizi wa biashara. Kampuni na taasisi za biashara zimekuwa na mahitaji makubwa kwa wahitimu wa kozi hiyo katika kusimamia biashara na hatimaye kuleta ufanisi.

Kimaro ambaye alihitimu shahada hiyo mwaka 2018 na sasa anafanya kazi CRDB kama Meneja Uhusiano Idara ya Mikopo, alisema aliamua kusoma kozi hiyo ili kupanua wigo wa kitaaluma na kufanya kazi kwa weledi.

"Baada ya kufanya kazi kama ofisa wa benki, hasa katika idara ya uendeshaji kwa miaka minane nikaona ni wakati mwafaka wa kuongeza kiwango changu cha elimu na ujuzi hasa katika eneo la usimamizi wa biashara ili kuendana na mahitaji ya taaluma yangu na tasnia ya benki inayobadilika kila mara. Lakini muhimu zaidi niliamua kuimarisha akili yangu na kujiandaa kuhudumu katika upande wa biashara katika kazi yangu," alisema.



"Kozi hii ya Usimamizi wa Biashara imenisaidia kupata ujuzi hasa katika uhasibu, usimamizi, sheria ya biashara na masoko. Pia imesaidia kuboresha uwezo wangu kifikra na kunitayarisha vyema katika kufanya kazi kwenye tasnia ya benki ambako kunahitaji ubunifu na ujuzi. Muda mwingi ninakutana na wateja na jukumu langu kubwa ni kutoa suluhu kwa maswali ya wateja kuhusiana na biashara," aliongeza.

Pamoja na mafanikio hayo, Kimaro alishauri NIT kuongeza udahili kwa wanawake katika programu zake ili kukuza na kuboresha uwezo wao katika kuwatayarisha kushindana na kunyakua fursa mbalimbali za kiuchumi na kuwa wachapakazi zaidi.

Kutokana na mafanikio aliyoyapata mpaka sasa, alisema malengo yake ya muda mrefu ni kutamani nafasi ya juu ya usimamizi uongozi katika benki au asasi nyingine yoyote ya wafanyabiashara wakubwa, kujifunza ufundi stadi ili kujiandaa na majukumu ya uongozi na kuwaandaa wengine.

"Ninajipanga kuongeza ujuzi wa elimu zaidi kwani ni muhimu na pia natamani kuwa katika majukumu makubwa ya uongozi iwe katika tasnia ya benki, serikalini au shirika lolote linalojihusisha na biashara.

# MAISHA

SEPTEMBA 24, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*


Ukurasa 12




## HARUSI

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



Tumia gharama kidogo kubadili mwonekano wa nyumba yako




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# IFAHAMU NGOZI YAKO

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | | O | M | B | W | A |
| H | | | | W | | O |
| U | | F | I | A | | K |
| K | U | U | | W | A | O |
| U | | N | O | A | | T |
| R | | D | | | | W |
| U | K | A | T | A | | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


PEN, SAA, GAO, NOA, PASHA, GONGA, PIGWA, AJABU, SHINDWA, ASHONWE

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI

SEBULE YETU IMEVAMIWA NA PANYA 18... HEBU WATAFUTE TUWAONE!



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

WATOTO wawili Juma na James walikuwa wakienda porini kutafuta vipepeo.

Walipokuwa porini Juma na James walianza kufundishana namna ya kuwakamata vipepeo bila ya kuwadhuru.

Juma: Niliambiwa na mama kuwa vipepeo ni viumbe vizuri

James: Hata mama yangu aliniambia lakini alisema ni dhaifu wakati wa kuwakamata.

Juma: Kama ni dhaifu kwa nini tumekuja kuwakamata? Ni bora kuwaacha tu kwani tutaonekana sisi sio majasiri.

James: Sina maana hiyo, yaani mbawa zake zinatoka kwa urahisi.

**SWALI**

Kilimo cha miti ya mbao kinapatikana mkoa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mkwe anapotiliwa shaka mimba kuharibika!

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kuelimishana kuhusu yanayoendelea katika familia zetu kila uchao. Wiki iliyopita niliahidi kutoa simulizi fupi mwanamke anavyomnyima raha mumewe kwa tabia ya kutimkia kwao mara kwa mara.

Nikasema hao ni wanawake mwiba kwa waume zao! Hata hivyo, ikabainika kwamba hadi kufikia hatua hiyo, kumbe yalikuwa maelekezo ya mama yake mzazi mwenye viashiria vya ushirikina. Kwa nini mimba za binti yake huyo ziliharibika kitatanishi?

Hebu msomaji wangu pitia na wewe ujumbe huu ambao baba mmoja alinitumia kupitia simu ya kiganjani kuelezea masikitiko yake ya kile kinachomsibu. Ukiona mwanamume amepaza sauti, ujue yamemfika shingoni.

Si unajua wanaume ni wagumu na wavumilivu fulani wanapokumbana na jambo zito? Wanayo ile nguvu ya kujizuia kuliko ilivyo kwa wanawake wengi.

Mwanamke atalia kwa kujigaragaza lakini mwanamume atainamisha kichwa chini na kutoa machozi anayojaribu sana kuyazuia, tena bila sauti ya juu. Ukiona mwanamume anatoa siri zake za ndani, hapo amefikia mwisho kwamba acha na ijulikane.

Ujumbe wa msomaji huyu mzuri wa safu hii ukasomeka hivi: “Maisha Ndivyo Yalivyo dada Flora. Kuna wakwe wewe mwenyewe utasema basi, liwalo na liwe kwa vituko unavyoshuhudia katika maisha yako.

“Mimi nina mke na mtoto mmoja. Lakini tatizo la mke wangu ni mimba kuharibika. Nikaenda hospitali mbalimbali bila kujua chanzo. Na wakati huo tayari zilishaharibika mimba sita. Madaktari hawaoni tatizo ni nini lakini mimba ikifika miezi mitatu inatoka!

“Nikaona ngoja nimshirikishe mama mkwe anipe wazo kuhusu tatizo hili kwa mke wangu. Jibu nililopewa mpaka leo sina hamu naye. Bado nawaza wala sipapati jawabu la kuponya nafsi yangu.”

Baada ya ujumbe huu hata mimi nilitafakari kwa kina. Lakini ilibidi nimtafute baba huyu kwa simu kumuuliza maswali kadhaa kwa ufafanuzi zaidi kuhusu kile anachopitia.

Nilipomdadisi zaidi akasema yafuatayo kwamba ndivyo mama mkwe aliyomjibu; “Unahangaikia watoto? Kwani watoto ni nini!” Jibu hili lilimshangaza sana kwani lilizidi kumwumiza badala ya kumtia moyo.

Anasema kilichofuata baada ya hapo ni vituko vya mke wake alivyokuwa akipanga safari za mara kwa mara kwenda kijijini kwao aliko mama yake. Naweza kuwa nimekwenda kwenye shughuli zangu za biashara, tunaagana vizuri na kuondoka.

Lakini ninaporejea jioni mwanamke hayupo. Nikimtafuta kwa simu hapokei jambo ambalo lilikuwa likinipa wasiwasi sana. Inapofika majira ya usiku ndipo yeye hunipigia na kuniambia kwamba yuko kwao, hivyo nisimtafute. Nikimwuliza kuna nini anadai mama yake alikuwa hajisikii vizuri, hivyo akamhitaji aende kumwona. Maadam imeshatokea mimi nakuwa mtulivu kwani kubishana sana na mwanamke sina hulka hiyo. Ondoka yake hiyo si kwamba atarejea mapema bali amekuwa akikaa kwao takriban miezi mitatu.

Muda huo umekuwa ukijirudia mara kadhaa yaani hukaa huko kwao miezi mitatu kila aendapo. Ilifikia wakati mke wangu ananishawishi nihamishie shughuli za biashara huko kwao. Nilipodadisi zaidi nikagundua kuwa mama mkwe anajihusisha na vitendo vya kishirikina.

Na jibu hilo nimelipata baada ya kwenda kwa wataalamu (waganga wa kienyeji) wasiozidi watatu huku wakinipa majibu yanayofanana kwamba mkwe wangu ni mshirikina na hata mimba zinazoharibika ndiye mhusika mkuu. Nilishangaa sana.

Nikawaza kwa nini mke wangu na mama yake walikuwa wanasisitiza nihamishie shughuli huko kwao. Hata hivyo, nilimwambia mke wangu wazi kwamba siondoki mjini kwenye biashara kujikimu kimaisha.

Msomaji wangu, hayo ndiyo yanayomsibu ndugu yetu huyo. Wanaoingia kwenye ndoa hukutana na wakwe wa aina mbalimbali. Wengine wacha Mungu, wengine waabudu mizimu, matambiko, wenye roho za kichawi na kadhalika. Sasa utakapokuwa na wakwe ambao hawajaokoka, usifanye kosa la kuhukumu matendo yao na misingi yao ya kidini.

Kumbuka kwamba wanamhitaji Mungu na matendo yako wewe ndiyo yanaweza kuwabadilisha. Kumbuka siku zote kuwa mambo mengine wanayafanya kwa sababu ya kutofahamu (ujinga).

Mwombe Mungu akupe hekima jinsi ya kuchukuliana nao. Waonyeshe tunda la roho la upendo ili uweze kuwavuta wamjue Mungu. Kuwa mwangalifu na makini, usishiriki ibada zao za sanamu kama kutumia hirizi, dawa za kienyeji na matambiko.

***Je, una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Kwenye afya ndiko tunakouona ufukara usiopakwa rangi-2

KUNA ngonjera nyingi kuhusu ‘Toto Afya Card’ zinaendelea huko kwenye mitandao ya kijamii na kwenye majukwaa ya wanasiasa. Kila mmoja anataka hoja yake isikilizwe na maoni yake yajumuishwe kwenye mpango.

Hii haiwezekani ingawa kuna hoja za msingi ambazo zinapigiwa kelele kwamba zinahitaji maboresho. Ni muhimu serikali ikasikiliza watu wake, isiwaamulie kila kitu.

Hili la Toto Afya Card itazamwe upya na ikiwezekana mpango ulegeze gharama za uchangiaji.

Gharama za uchangiaji ni kubwa na mwananchi wa kawaida ni ngumu kumudu kutokana na kupaa kwa gharama za maisha.

Ni mwendawazimu peke yake anayeweza kuamini kwamba anaweza kuitelekeza afya yake kwa matarajio kwamba dola au jamii, au mtu mwingine atajali na kuishughulikia.

Aidha, ni mwendawazimu huyo huyo, anayeweza kufikiri kwamba kila mtu akijali afya yake binafsi, tutakuwa tumemaliza matatizo ya afya ya jamii. Lahasha iko nguvu ya umma inahitajika!

Mwanzo kabisa, nilichapisha waraka huu, ukihusu kujadili mtizamo hasi wa baadhi ya watu, kusita au kupuuza suala la kuchunguza afya zao na hasa ugonjwa wa kifua kikuu, unaosababishwa na bakteria maarufu ‘mycobacteria tuberculosis.’

Ugonjwa huu wa kifua kikuu, huathiri mapafu, mishipa ya fahamu, mifupa, mfumo wa mzunguko wa damu, ngozi, viunganishi vya mifupa na lymphatic system. Virusi hivyo viligunduliwa na mwanasayansi wa Ujerumani, Robert Koch, mwaka 1882.

Siku hizi kuna watoto wenye umri chini ya miaka 18 wana maambukizi ya TB ndiyo maana tunatamani gharama zipungue na masharti yalegezwe ili kila mtoto apate huduma za afya bila kikwazo.

Katika hali hiyo, ni dhahiri kwamba tunahitaji nguvu ya pamoja, kwa maana ya utashi wa umma wenyewe katika kuinua kiwango cha elimu na uelewa wa kutosha wa wananchi wake kuhusu masuala ya siha ya umma wa Watanzania na kuwekeza zaidi katika jitihada za makusudi.

Ni lazima sasa tuwe na kampeni za kudumu za kuwahamasisha Watanzania na kuwakumbusha kuhusu umuhimu wa kufanya uchunguzi wa afya zao mara kwa mara. Ngoja niwaambie ukweli pasina shaka kwamba bado hatujawekeza ipasavyo katika siha yetu kama taifa.

Kwa mfano, takwimu zinaonyesha kwamba tumepunguza maambukizi mapya ya kifua kikuu kutoka wagonjwa 306 katika kila idadi ya watu 100,000 na kufikia wagonjwa 208 katika kila watu 100,000 ikiwa ni sawa na kupungua kwa asilimia 32.

Katika Hospitali Maalum ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong’oto, kanzidata yake inaonyesha kuwa asilimia 70 ya wagonjwa wanaolazwa wodi moja katika hospitali hiyo wanatumia hewa tiba ya Oksijeni. Kwamba huduma hiyo wodini inawahusisha wagonjwa kati ya 20 hadi 30, ambapo gharama kwa mtungi mmoja wa Oksijeni kwa sasa ni zaidi ya Sh. 45,000.

> **Hili la Toto Afya Card itazamwe upya na ikiwezekana mpango ulegeze gharama za uchangiaji.**

Maana yake nini? Iko haja ya kuanzisha kampeni ya kitaifa kama tunavyoweka nguvu kubwa hivi sasa katika kutoa elimu kuhusu mlipuko wa ugongwa wa ‘Marburg’ ulioua watu sita na wengine watatu kulazwa huko mkoani Kagera. Watanzania wapewe elimu bila kujali gharama, lasivyo, tutapoteza idadi kubwa ya watu wetu.

Ziko tafrisi nyingi, lakini mojawapo ni kwamba idadi kubwa ya Watanzania, hasa walioko vijijini na pembezoni, hawajafikiwa na elimu ya kutosha kuhusu TB. Wengi wanaoishi huko, ndiko tunakoona ufukara kwa uhalisia, usiopakwa rangi. Huko ndiko waliko wazalishaji wakuu wa pato la taifa.

**• Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com simu ya mkononi: +255 767 535490**


# HARUSI








SEPTEMBA 15 ILIKUWA SIKU YA FURAHA KWA SALUM KALYANYE NA JACKLINE BAADA YA KUFUNGA NDOA NA KUWA MUME NA MKE. MAHARUSI HAO AMBAO WANAISHI OHIO NCHINI MAREKANI WALIFUNGA NDOA HIYO KATIKA UKUMBI WA MSASANI TOWER MKOANI DAR ES SALAAM.





# MITINDO







## USIHOFU UNENE Vaa hivi utapendeza

KUNA dhana kwamba wanawake wanene si wazuri kwa mwonekano, lakini hii si sawa kwa sababu pia nao wanapendeza.

Kutokana na fikra hizo, baadhi ya wanawake wenye miili mikubwa wamejikuta wakipoteza fedha nyingi kwa ajili ya kupunguza.

Wakati mwingine wanatumia dawa zenye kemikali ili kuondokana na tatizo hilo.

Kibaya zaidi hukata tamaa hasa linapokuja suala la mavazi, wanashindwa kujiamini kama kuna nguo zinawakaa vizuri na kutoka bomba.

Wenye tatizo hilo ni lazima kujiamini na kuwa na furaha kwa sababu suala la mavazi kwao liko vizuri.

**MAVAZI SAHIHI**

Chagua nguo zinazolingana na mwili wako kwa sababu siri ya kupendeza ni kuvaa nguo inayokutosha vizuri.

Epuka kununua nguo zinazokubana sana ili kuondoa alama ya mikunjo ya mwili kuonekana.

Aidha epuka kuvaa nguo pana zaidi ili kutoonekana na umbo kubwa zaidi ambalo litakupa mwonekano mbaya.

Si lazima utumie fedha nyingi kununua mavazi, kikubwa tumia ubunifu wakati wa kununua nguo hata kama za mitumba.

URUMBO

**Na Mary Geofrey**

# IFAHAMU NGOZI YAKO

VIPODOZI vinatumika na watu wengi kama njia mbadala ya kurembesha sura na utunzaji wa ngozi.

Kuna aina mbalimbali ya vipodozi ambavyo vimetengenezwa na mchanganyiko wa misombo kwa ajili ya kufanya kazi katika ubora.

Leo tutaangalia matumizi ya poda katika kuboresha ngozi.

Jinsi ya kuchagua poda inayokufaa

Kwa wenye ngozi nyepesi, wanashauriwa kuchagua rangi ya pinki kwa mbali.

Kwa rangi iliyokolea ya ngozi, inashauriwa kuchagua rangi ya njano au ya machungwa, ambayo inafanana kabisa na rangi ya awali ya ngozi.

Kwa ngozi ya kung'aa unashauriwa kuchagua poda kahawia kwa sababu hurekebisha ngozi isiyo na usawa na husaidia kufunika rangi isiyohitajika.

Ngozi kavu

Kwa watu walio na aina ya ngozi kavu, poda ya kumaliza ukavu haifai kwa sababu inaweza kufanya ngozi kuwa kavu zaidi.

Na hata kuchagua poda ya uso iliyo na krimu au poda ya kurekebisha isiyo na mwanga.


Aidha, poda zenye viambato kama vile Vitamini E ndizo zinafaa kwa ngozi yako.

Ngozi ya mafuta

Kwa watu walio na aina ya ngozi ya mafuta, poda ya kumaliza unyevu ni bora kwa kuzuia uzalishaji wa mafuta ya ziada.

Ni lazima mtu aepuke poda zinazong'aa kwani zinaweza kufanya uso uonekane una mafuta.

Mwenye ngozi ya mafuta hakikisha unasugua uso wako taratibu na vipande vya barafu, kabla ya kuanza kujipodoa husaidia kudhibiti uzalishaji wa mafuta kupita kiasi na kupunguza vinyweleo.





MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Furahia juisi ya lozera

JUISI ya Lozera ni moja kati ya vinywaji maarufu katika maeneo mengi nchini.

Ubunifu zaidi umeongezwa katika kinywaji hicho, kwa sasa huchanganywa na matunda mengine kama nanasi, chungwa, pasheni, limao, ubuyu pamoja na viungo mbalimbali.

Wataalamu wa afya wanasema utumiaji wa juisi hii unaweza kuongeza damu ikiwa utatumiwa mfululizo kwa angalau wiki mbili

**Maandalizi**

Baadhi ya watu huyaloweka majani ya lozera kwa muda mfupi kisha huchuja na hapo inakuwa tayari kwa kunywa lakini leo tunaangazia njia nyingine ya kuchemsha.

Hatua ya kwanza ya uandaaji wa juisi ya lozera ni kuandaa jiko utakalotumia kuchemshia kinywaji hicho kisha bandika maji kiasi kutokana na wingi wa majani ya lozera uliyonayo kisha yaache yapate moto kidogo.

Maji yakishapata moto, weka majani ya lozera kiasi upendacho, ongeza maganda ya nanasi, tangawizi, mdalasini na iriki kama unapendelea, kisha acha yachemke.

Ili kufurahia utamu wa juisi ya lozera baadhi ya wapishi na wauzaji wa kinywaji hicho wanashauri kuchemsha kwa muda mfupi ili kuepuka juisi hiyo kukosa ladha.

Ukiona majani ya lozera yamebadilika rangi na kuwa ya pinki hivi au ile rangi yake ya kukolea imepungua basi ujue hapo ipo tayari.

Hatua inayofuata baada ya kuchemka ni kuchuja na kuongeza sukari au asali kama unapendelea na juisi yako itakuwa tayari kwa kunywa.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Tumia gharama kidogo kubadili mwonekano wa nyumba yako

BAADA ya miaka kadhaa ya kuishi kwenye nyumba, wengi hutamani kubadilisha mwonekano.

Na mara nyingi wamiliki wengi wa nyumba hupendelea kurekebisha jengo au kununua samani mpya ambazo hutumia gharama kubwa.

Andiko hili la leo ni kukupa mwanga tu namna ya kuboresha maisha ya nyumbani kwako kwa gharama nafuu na ukabaki unafurahia maisha.

Kumbuka kwamba si tu matumizi makubwa pekee ya pesa ambayo yanaweza kubadilisha au kuleta mvuto wa nyumba, bali hata kwa gharama kidogo tu ya pesa hiyo ina uwezo wa kuipendezesha.

Kwa mfano matumizi tofauti ya rangi, karatasi za ukutani, vitambaa na malighafi zingine zilizotengenezea samani zako, vina nafasi kubwa ya kubadilisha kabisa mwonekano wa nyumba yako na kukupa wa kuvutia zaidi.

Kwa mfano kupaka rangi upya kabati la luninga, miguu ya kiti au meza, kubadili kitambaa kilichotengenezea viti au sofa, nako kunasaidia kubadilisha muonekano katika nyumba yako.

Nyingine ni kubadili vitu kidogodogo kama vile tai na fimbo za pazia, pazia zenyewe, zuria, mapambo ya ukutani na mengineyo.

Viko vitu vingi ambavyo unaweza kuvifanyia marekebisho kwa gharama ndogo ndani ya nyumba yako na ukaifurahia tena na usiichoke, kwa mfano kubadili rangi ya



ukuta nayo ni mbinu nyingine.

Pia hata kuchagua kubadili kitu kingine unachoona unatakiwa kufanya hivyo. Kama ni foronya unatakiwa kuangalia zile zinazoendana na zilizoko kwa wakati wa sasa.

Kama vitu vyako vya ndani umevitumia kwa miaka mingi na vimepitwa na wakati na ndiyo maana huenda vinakuchosha na kuiona nyumba yako mbaya, usiikatie tamaa kwa sababu inawezekana kuirudisha katika ubora wake.

Kikubwa ni kuwa mbunifu na kuongeza kidogokidogo vionjo vinavyoendana na wakati katika nyumba yako hiyo, hata kama huna kipato kikubwa inawezekana. Si lazima uweke vyote kwa pamoja, lakini kadri unavyojaaliwa unabadili cha zamani na unaweka kinachoendana na wakati wa sasa.

Utanunua pazia leo lakini siku nyingine kitu kingine na hii pia itasaidia nyumba yako kuonekana mpya kila siku.

Ni ukweli kuwa vitu vya nyumbani vinabadilika kila baada ya kipindi fulani, zuria ulilonunua miaka mitano iliyopita, haliwezi kuendana na wakati huu.

## Raha ya rangi mchanganyiko

**Na Restuta James**

PAMOJA na kwamba rangi nyeupe ndio pendwa zaidi katika nyumba nyingi, ukuaji wa teknolojia umeleta ubunifu wa kuchanganya rangi na kuongeza mvuto ndani ya nyumba.

Kuchanganya rangi kwa kompyuta kumeongeza wigo wa uchaguzi wa rangi, kiasi kwamba kwa mwonekano mtu anaweza kufikiri nyumba ni nyeupe kumbe sivyo.

Wataalamu wa mapambo wanaeleza kuwa uchanganyaji wa rangi umesaidia kunogesha nyumba ndani na nje, na katika uzio.


Wanaeleza kuwa jambo la muhimu la kuzingatia ni kupaka rangi inayong'aa katika ukuta mkubwa na nyingine kwenye kuta ndogo hususani zinazotenganisha dirisha au karibu na mlango.

"Kwenye vyumba vya watoto wa kiume wengi rangi pendwa ni bluu lakini inaweza kuchanganywa na ikapatikana bluu tulivu au kijani tulivu wakati vyumba vya watoto wa kike rangi nzuri ni pinki tulivu na zambarau," anaeleza mtaalamu, Diana Mwaikambo.


Anataja mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kununua rangi ni kuangalia rangi pendwa na kwamba hata dari si lazima kupaka nyeupe kwa kuwa uchanganyaji wa rangi kiteknolojia unaweza kumpatia mteja mwonekano wa tofauti.

"Rangi zinaleta umaridadi kwenye nyumba, kuathiri fikra zako na matendo yako, ni muhimu sana kuchagua rangi itakayotuliza hisia zako uwapo nyumbani," anasema.

Diana anasema kuwa rangi ya njano ya dhahabu na nyeupe ya kijivu ni rangi 'zinazokamilishana.'



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
NIMEACHA MKE ASUBUHI MCHANA KAOLEWA NA MPANGAJI MWENZANGU!
JUKWAANI
MUDA WA MIMI KURUDISHA AFYA NA KUWA BONGE NDIO HUU
NIHURUMIE MIMI NI MGOMBEA USO UMEUMBWA NA HAYA LAKINI ZILE CHALE HADI NIMEENDA KUSHONWA SHIKA ADABU YAKO!
WEWE NDIO ULIYESEMA KUWA KWA KIINUA MGONGO UTATOBOA?
NENDA BAR NILIYOTOKA UKASHUHUDIE 'NILIVYOTOBOA' CHUPA ZAO
ABIRIA ANZISHENI MAPAMBIO MANAKE MSIBA TAYARI...!
KAMA YEYE ANALIPULIZA MIMI MWENZIE NALITAFUNA
MIKOPO AMBAYO OFISI ZAKE ZINATAZAMANA NA BAR INATUPA MITIHANI WENZENU JAMANI!
HAWAVUMI
SOKONI
MKE NILIYEMUOA KAINGIZA BWANA CHUMBANI KWANGU
KATAFUTE MASELA WAPELEKE WAKAMALIZE KESI
UNASEMAJE MUME?
WASINGENIAMULIA UNGESIKIA NISHAUA JITU ULINGONI
*KINYUNYIZO CHA LEO...
'NJIA PANDA HAITOSHEKI KUVUNJIWA NAZI...

## HABARI KIMATAIFA

# Jenerali Al Burhan akubali mazungumzo

**KHARTOUM,** SUDAN
KIONGOZI wa Jeshi la Sudan Jenerali Abdel Fattah al Buhan, amesema yupo tayari kuzungumza na kamanda wa vikosi vya Rapid Sapport Forces (RSF) Mohamed Hamdan Dagalo, kwa ajili ya kumaliza vita.

Wawili hao wamekuwa wakipambana vikali katika vita vya ndani tangu Aprili.

Umoja wa Mataifa umeeleza mapigano hayo yamesababisha vifo vya zaidi ya watu 5000 na wengine zaidi ya milioni tano wameachwa bila ya makazi.

Jenerali Burhan, alikuwa akizungumza na BBC katika mahojiano baada ya kuhutubia Baraza Kuu la Usalama mjini New York.

Jenerali Al-Burhan analiongoza jeshi la Sudan na anafanya ziara ya kidiplomasia ya kimataifa akitafuta uungwaji mkono, licha ya kushindwa kukabidhi madaraka kwa utawala wa kiraia.

Kiongozi huyo wa jeshi alikana kikosi chake kinawalenga raia, licha ya Umoja wa Mataifa na mashirika ya misaada kusema kwamba kuna ushahidi kuwa wanarusha makombora yanayolenga makazi ya watu.

Burhan alisema ana imani atapata ushindi, lakini amekiri kwamba amelazimika kuhamisha makao yake makuu hadi Port Sudan kwa sababu vita katika mji mkuu Khartoum imeweka ugumu kwa serikali kuendelea na shughuli zake.

Aidha, alisema atakaa chini na Jenerali Dagalo anayefahamika kama Hemedti ili mradi atimize ahadi ya kuwalinda raia iliyotolewa na pande zote katika mazungumzo yaliyofanyika Mei katika mji wa Jeddah, nchini Saudi Arabia.

Katika ujumbe wa video uliotolewa wiki hii Hemedti alidai kuwa yuko tayari kufanya mazungumzo ya kisiasa.

Pia Jenerali Burhan alikanusha kuwa Sudan itaingia katika ,mfumo wa utawala ulioshindwa kama Somalia au nchi iliyogawanyika ya Libya.

**BBC**



Papa Francis akizungumza kwenye kongamano la Kanisa Katoliki juu ya masuala ya Bahari ya Mediterenia lililofanyika Marseille, nchini Ufaransa juzi. **PICHA: AP**

# Papa Francis ahofia Mediterenia kugeuka kuwa bahari ya mauti

**PARIS,** UFARANSA
KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, amelaani kile alichokiita uzalendo wa uadui na kutaka nchi za Ulaya kushughulikia suala la wahamiaji ili kuzuwia kuigeuza Bahari ya Mediterenia kuwa kaburi la watu.

Papa Francis aliyazungumza hayo kwenye hotuba yake ndefu ya kuunga mkono wahamiaji wanaoingia barani Ulaya iliyohitimisha kongamano la Kanisa lake kuhusu masuala ya Bahari ya Mediterenia mjini Marseille nchini Ufaransa.

Mji huo wa bandari kwa karne kadhaa umekuwa sehemu ya mkusanyiko wa kongamano la tamaduni na dini mbalimbali.

"Kuna kilio cha maumivu kinachotugusa sote, na kinaibadilisha Mediterenia, bahari yetu, kutoka kuwa chanzo cha ustaarabu na kuwa, bahari ya mauti, ni kilio cha masikitiko cha kaka na dada zetu wahamiaji", alisema.

Papa Francis alipokelewa kwenye mji huo na Rais Emmanuel Macron ambaye baadaye jana walipangiwa kuwa na mkutano wa faragha.

Katika ziara yake hiyo alianza kwa kukitembelea kituo kinachowahudumia wenye mahitaji katika wilaya ya Mtakatifu Mauront, mojawapo ya maeneo masikini nchini Ufaransa.

Baadaye kwenye kongamano hilo, alitoa wito wa kuwepo kwa njia nyingi, za kawaida na za halali kwa wahamiaji, akisisitiza kuwakubali zaidi wale wanaokimbia vita, njaa na umasikini kuliko kuwakataa.

Kwa mujibu wa Shirika la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR), wahamiaji wapatao 178,500 wameingia barani Ulaya kupitia Bahari ya Mediterenia mwaka huu, huku wengine wapatao 2,500 wakifa au kupotea baharini.

Serikali za mataifa kadhaa ya Ulaya, zikiwemo za Italia, Hungary na Poland, zinaongozwa na viongozi wanaopinga wahamiaji.

Papa Francis alitoa wito kwa watu kuvisikia vilio vya maumivu vinavyopazwa kutoka Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati.

"Katika muda kama huu ambao tunahitaji makutano haya, pale uzalendo wa uadui na usio wa maana unapotaka kuifanya ndoto ya jamii ya mataifa kufifia," alisisitiza kiongozi huyo.

**DW**

# Ukraine yashambulia meli za Russia

**MOSCOW,** RUSSIA
UKRAINE imefanya shambulio la makombora na kuharibu meli za Russia zilizopo Bahari Nyeusi katika jimbo la Crimea.

Katika tukio hilo, mwanajeshi mmoja amepotea baada ya shambulio hilo la kombora, kulingana na mamlaka ya Russia.

Meli hizo zimekuwa ni shabaha kwa vikosi vya Ukraine kutokana na kuwa bora zaidi katika jeshi la wanamaji la Russia.

Ukraine ilifanya mashambulizi kadhaa Crimea hivi karibuni, ikiwa ni pamoja na kushambulia mfumo wa ulinzi wa anga na meli mbili za majini.

Kutokana na hali ya shambulio hilo, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky alitembelea bunge la Canada kutoa hotuba ambapo aliishukuru Canada kwa kuwa mfano kwa wengine kote ulimwenguni katika uungaji mkono wake kwa nchi yake.

Alisema Canada imekuwa nyumbani kwa raia wa Ukraine na kuahidi watakuwa washindi, huku nchi yake inaweza kuomba uungwaji mkono kwa vile inataka kuokoa maisha ya mamilioni ya watu wake.

Waziri Mkuu wa Canada Justin Trudeau aliahidi msaada zaidi wenye thamani ya dola za nchi hiyo milioni 650 ikijumuisha magari 50 ya kivita na mafunzo kwa marubani na wahandisi wa ndege za kivita za F-16.

Wakati huo huo, Rais wa Marekani Joe Biden anatarajia kuipatia Ukraine makombora ya masafa marefu ili kuisaidia kukabiliana na mashambulizi yanayoendelea.

Maofisa wa Marekani wanaofahamu suala hilo walisema Ukraine itapata makombora ya ATACMS yenye masafa ya hadi maili 190 kwa sasa.

Hii itaiwezesha Ukraine kushambulia vikosi vya Russia vilivyo nyuma ya mstari wa mbele.

**BBC**

## MAKALA

# MAISHA YA NDOA HAYAFANANI, TUWE MAKINI KUHUSU ELIMU ZITOLEWAZO



Na Magabilo Masambu

UNAPOSIKIA neno ndoa kwa dini, mila na desturi zetu za kitanzania, ina maana ni muungano kati ya mwanamume na mwanamke.

Yaweza kuwa ya kanisani, kiserikali au ya kimila, hizo zingine waachiwe wenyewe watajuana na muumba wao siku ya hukumu.

Hivi sasa kumeibuka utamaduni wa baadhi ya watu katika mitandao mbalimbali ya kijamii kutoa elimu au mafundisho yanayohusu ndoa kama ambavyo zinatolewa elimu nyinginezo za dawa na kadhalila.

Wako baadhi ya wanandoa pia ambao wanashinda mitandaoni, wakijifunza namna ya kuendesha maisha yao ya ndoa kupitia mafunzo hayo. Si jambo baya lakini Jakaya Kikwete, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, aliwahi kusema akili za kuambiwa changanya na zako, tusiwe kama king'ota.

Wako watu wanasema ndoa ni ya kipekee na kwamba haiwezi kufanana na nyingine. Nakubaliana nao kwa sababu, kwanza, changamoto zinatofautiana, watu wanatofautiana, vipato vinatofautiana, nauelewa pia ni tofauti.

Familia walikotoka zina desturi na utamaduni tofauti, malezi hayafanani. Mambo yote yanatofautiana sasa kwa nini utumie elimu yenye uzoefu fulani tu halafu kisha ndiyo uifanye mwongozo wa ndoa yako?

Nilichogundua ni kwamba baadhi ya wanaotoa elimu za ndoa katika mitandao ya kijamii, wengi wao ama wameachika au wameacha na wanatumia udhaifu wa wenza wao kufundisha kuhusu ndoa bila wao kusema ukweli juu ya makosa waliyowatendea wenzi wao.

Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere katika kitabu chake cha Tujisahihishe, anasema kila binadamu anayo tabia ya unafsi, nayo ni kusema mabaya ya wengine na kuficha mabaya yake.

Yaani wewe ndiye mkosaji, lakini husemi makosa yako badala yake unasema mazuri yako na kusema mabaya ya wengine kwa watu.

Kujaribu kuishi maisha ya ndoa nyingine usiyofahamu kwa nini wao wanaishi vile wanavyoonekana ni kujaribu kuvunja ndoa kwa mikono yako mwenyewe.

Kuchukua ushauri wa mtu ambaye hasemi makosa yake, badala yake anasema ya mwenzake ni hatua mojawapo kuelekea kuvunja ndoa yako. Kuiga maisha yasiyo yako umeona kwa jirani ni kujifunza kwa vitendo bila kufundishwa. Kulinganisha mume au mke wako na wa jirani na kutamani maisha yao ni mwendelezo wa kupata elimu ya kuvunja ndoa yako bila mwalimu.

Swali je, sasa watu wasijifuze? Jibu langu ni kwamba kila unachokiona ni elimu kwako tofauti yako na mbuzi ni utashi. Kwa hiyo unalazimika kuamua kama kila unachokiona utakichukua na kukitumia au utakiacha kiende zake. Tunaweza kutazama kila kitu lakini ni muhimu kuchambua cha kuchukua na kuacha kwa maslahi ya maisha yetu.

Kuna watu wanaajiriwa mwaka mmoja mshahara unafanana, lakini baada ya muda fulani maisha yao hutofautiana. Usilazimishe kila alicho nacho mwenzako uwe nacho na wewe una wakati wako.

Wenza wasipolijua hili wakaenda kusikiliza kwa walimu wa mitandaoni ndoa inavunjika. Maisha ya ndoa yana siri kubwa sana.

Kuna watu wanaonekana barabarani kila mahali wakiambatana na kwamba wanaonekana wanandoa wa mfano, kumbe ndani kila mmoja ana chumba chake. Hayo hawatayasema kwa sababu ile ya unafsi.

Kuna baadhi ya hao walimu wa ndoa sasa wanahamasisha watu kuachana.

Ni kweli nakubali kwamba kuna baadhi ya mambo hayavumiliki kwenye ndoa, lakini usimwache mwenzako kwa sababu umepata ushauri kwa mtu.

Fanya hivyo kwa sababu wewe mwenyewe umeona huwezi kutoboa, mkiachana kwa ushauri wa mtu iko siku mtamlaumu huyo mtu.

Wengi wanaohamasisha wanajikita kwenye suala la kipato yaani ndoa sasa umekuwa mtaji.

Watu hawafikirii namna ya kujikwamua kiuchumi kwa kushirikiana bali wanaona mmoja kati ya wawili ndiye anayetakiwa kuhakikisha kila kitu kinapatikana, lakini wakifikia wakati wa kuachana, wanakwenda kudai mahakamani kwamba walitafuta pamoja!

Suala la ndoa hata baadhi ya wanasaikolojia waliokaa darasani na kusomea masuala hayo ya uhusiano pamoja na elimu nzuri sana wanayotoa, bado wao wenyewe kuishi mafundisho yao ni taabu. Pengine ndiyo yale maneno ya wahenga kwamba mganga hajigangi.

Hii inathibitisha kwamba, hakuna mwalimu aliyekamilika katika maisha ya ndoa.

Kuna watu hawana vipato kwenye familia, ndoa zinavunjika kwa kisingizio cha ugumu wa Maisha.

Kuna watu wanapata kila kitu wanachokihitaji kwa kuwa wana kipato kizuri lakini bado ndoa zinavunjika. Angalau kidogo wasiokwenda shule kabisa na hawana kipato kizuri ndoa zao zinaonekana kuwa imara. Kama ni kujifunza basi tunaweza kufahamu siri ya urembo.

Sina hakika kama na mimi nilikuwa natoa elimu ya ndoa lakini lengo kubwa hapa ni kutahadharisha juu ya kutumia uzoefu na makosa ya watu wengine kuendesha familia zetu. Kama jambo huna uwezo nalo ieleweke hivyo.

Kama kuna mtu anatamani vitu anavyovitazama barabarani mwache avifuate lakini huna sababu ya kufanya jambo lililo nje ya uwezo wako kwa sababu tu unataka mumeo au mkeo afurahi. Utakufa kabla ya siku zako.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Una uzuri gani mpaka uringe?



Na Adam Fungamwango

MARINGO, kupenda sifa na kiburi ni vitu vinavyokwenda sambamba. Kuna watu dunia hii unaweza ukadhani wameshushwa au kujiumba.

Utakuta baadhi ya watu wana viburi na kutesa wenzao kama vile ana ubia na Mwenyezi Mungu katika dunia hii.

Hawa ni wale ambao wana pesa, utajiri na madaraka. Baadhi ya wanasiasa nao wako radhi kufanya chochote na hata kukandamiza wananchi ambao wamewachagua.

Sasa wako wale ambao wanajiona 'mahendisamu' na 'masistaduu.' Usirogwe ukaingia kwenye anga za watu hawa.

Wanaringa kwa sababu ya kujaaliwa au kuambiwa kuwa ni wazuri. Kinachotokea ni kwamba wanajawa na kiburi, wanadharau watu wengine, wanachagua wa kuwasalimia, wengine wakionekana ni kama takataka.

Wanabagua watu wa kuongea nao, kuongozana nao na kikubwa zaidi watu wa ina hii huchelewa sana kuoa au kuolewa kwa sababu wanachagua sana wenza kwa sababu hizo hizo za uzuri au urembo wao. Masikini ya Mungu, wengi wao ni vijana sana na hawaijui dunia ilipotoka, ilipo na inapokwenda.

Dunia hii ya Mungu haina mzuri au mbaya, wote watapita raha na karaha. Haina tajiri wala masikini, kila mtu atapata amani na misukosuko. Dunia hii walipita watu wenye heshima zao waliokuwa waadilifu kwa Mungu, lakini wote hawa leo hawapo.

Kulikuwa na matajiri wa kila aina na wafalme wenye sifa na malkia wazuri, warembo, lakini leo hii wote wamewishaicha dunia ikisonga mbele. Mfalme Suleiman inasemekana kuwa ndiye alikuwa mtu tajiri zaidi duniani, busara na hekima nyingi lakini aliondoka.

Cleopatra, ndiye alikuwa mwanamke mzuri na mrembo kuliko wote duniani kwa wakati huo na inasemekana hadi leo hajazaliwa binti yeyote mwenye sifa na urembo kama wa kwake yeye. Pamoja na uzuri na urembo wake, alikuwa pia mtawala wa nchi ya Misri wakati huo, leo hii hayupo kwenye uso wa dunia.

Sasa mtu anapata wapi kiburi cha kujiona yeye ni mzuri na mrembo kiasi cha kudharau na kubagua watu wa kusalimiana nao, kutembea nao na hata wa kuongea nao?

Mwanamuziki David Amunga aliwahi kuimba wimbo mmoja na moja ya mashairi wake alisema, 'dunia uwanja wa fujo mwenye ngoma zake acheze zipasuke'. Na kipande hiki kilirudiwa na Marijani Rajab kwenye wimbo wake aliouita 'Dunia Uwanja wa Fujo.'

Maana wa nyimbo hizo zote ni kwamba binadamu hapaswi kuwatesa, kuwadharau, kuwabagua au kuwaringia wenzake kwa sababu hana uwezo wa kujiongezea hata sekunde moja ya kuishi duniani.

Uwe mzuri, tajiri, mrembo, lakini si kitu duniani hivyo binadamu wanatakiwa waishi kwa kupendana na kujaliana. Kwa sababu hata uwe tofauti na wenzako, lakini ipo siku utaumwa, utakufa na kuzikwa kwenye kaburi kama wenzako wote.

Ndiyo maana yeyote mwenye tabia ya maringo huwa hapendwi na jamii tangu zama hizo.

Mbaraka MwinsheheMwaruka alitunga kibao chake akakiita 'Uzuri si Hoja' na kukiimba na mzee Steve Hiza. Ni moja kati ya nyimbo zenye mafunzo kwa jamii.

"Hata uwe mzuri wa kupindukia, tabia yako ikiwa mbaya watakuchukia, hata mwendo urembeshe mithili ya twiga bila maelewano mapenzi hakuna kabisa, hata ujipambe kwa vito ung'ae kama nyota, pasipo tabia njema popote watakufukuza.

Kuishi na watu vema hutoharibikiwa, milele na milele watakukumbuka, heshima wapatie wote wadogo na wakubwa.

Kuishi na watu vema hutoharibikiwa, milele na milele watakukumbuka, heshima wapatie wote wadogo na wakubwa. Maisha ni tabia njema chochote utapata.

Heshima kijana, tanguliza kwanza mbele ujeuri mbaya hoho hoho. Heshima kijana, tanguliza kwanza mbele ujeuri mbaya hoho hoho.

Uzuri si hoja tabia njema ni silaha utapendwa popote hoho hoho. Uzuri si hoja tabia njema ni silaha utapendwa popote hoho hoho."

Hapa Mbaraka anatuambia kuwa ukiwa mwenye tabia njema unaweza kuishi na kupendwa popote na si mtu mwenye sura nzuri, maringo na jeuri.

Kwamba unajiuliza hivi kwa nini mtu anaringa? Ili iwe nini? Ikusaidie nini?

Kiko Kids iliyokuwa ikiongozwa na mkongwe Salum Zahoro nao walitunga wimbo wao wakauita 'Uzuri wako siutambui', ambao wengi wanaufahamu kwa jina la 'Kijana Sudi.'

Yeye akawa anamshangaa dada mmoja mwenye maringo, lakini kila akimuangalia hata uzuri ule ambao unamfanya awaringie watu.

"Ninapokuona hujiuliza moyoni mwangu mimi, uzuri wako siutambui mpaka kuringa wewe. Ninapokuona hujiuliza moyoni mwangu mimi, uzuri wako siutambui mpaka kuringa wewe.

Nitajaribu kumuuliza kijana Sudi wewe, anieleze kisa cha wewe mpaka kuringa wewe.

Nitajaribu kumuuliza kijana Sudi wewe, anieleze kisa cha wewe mpaka kuringa wewe."

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James.

# Kafie kwenu-12

Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

ALIPATA upinzani hata kwa dada yake ambaye alimshangaa na kumwona mtu asiye na kazi ya kufanya. Katika juhudi zake zote alipata watu wazima watano tu na yeye mwenyewe wa sita.

Wanafunzi 10, saba wa kike, akiwamo Saida na watatu wa kiume walijitokeza lakini kwa sababu walikuwa wadogo hawakuruhusiwa kuifanya kazi hiyo. Kazi ilianza kwanza ya kwenda kwenye kijumba chake ili kuangalia kama kuna nyaraka zozote ambazo ameacha.

Walipoona hakuna chochote cha kuwasaidia sasa ikaanza kazi ya kumsaka kwenye vituo vya polisi na hospitali zote za Dar ikiwamo kwenye vyumba ya maiti walau kupata hata mwili wake wauzike kwa heshima zote kama jirani yao.

Zunguka kote, wapi! Waliacha shughuli zao licha ya uchache wao wakamsaka James kama wanamsaka ndugu yao wa damu, ikashindikana. Wakanyoosha mikono juu. Wakamwachia Mungu.

"Kama atakuwa ameamua kwenda kokote kule kwa ajili ya kusaka maisha, Mwenyezi Mungu amjaalie. Kama amepatwa na kitu chochote kibaya na amepoteza maisha, Mwenyezi Mungu amweke mahala pema peponi." Ilikuwa kama sala ya mwisho, au neno la mwisho lililotolewa na Catty baada ya kikao chao kifupi na wote wakaitikia, "Amina."

Wale majirani sita waliojitolea kumsaka kila mmoja sasa akarejea kwenye maisha yake ya kawaida.

********************************

Miaka mingi iliyopita katika kijiji cha Mtakwenda mkoani Tabora alizaliwa msichana mmoja, wazazi wake wakamwita Farida.

Alilelewa kwa mapendo makubwa na wazazi wake walioendesha maisha yao kwa ukulima na ufugaji. Maisha yao mazuri yalianza kuingia dosari pale baba yake Farida, mzee Katandukila alipofariki dunia.

Maiti yake ilikutwa kwenye kisima, ikionekana kabisa ina mikwaruzo ambayo ilionyesha alikuwa anapambana na mtu.

Kijiji kiliitisha kikao ambacho mwenyekiti wake alibainisha kuwa kifo cha Katandukila inawezekana hakikutokana na kuanguka kwenye kisima kirefu alipokuwa akitoka kunywa pombe, bali aliuawa na mtu ambaye baada ya kutekeleza mauaji akaitumbukiza maiti kwenye kisima. Pamoja na hayo hakukuwa na uthibitisho wowote kuhusu hilo.




**"Mimi nilikuwa natoka kilabuni, nilipofika karibuni na kisima nikasikia chakara chakara. Na ulevi wangu wote kwanza akili ikanikaa sawa. Nikajificha nyuma ya mti, nilijua labda kuna mnyama.**

Alikuwepo mwanakijiji mmoja tu Chambanenge ndiye aliyedai ana ushahidi kuwa Katandukila aliuawa.

"Mimi nilikuwa natoka kilabuni, nilipofika karibuni na kisima nikasikia chakara chakara. Na ulevi wangu wote kwanza akili ikanikaa sawa. Nikajificha nyuma ya mti, nilijua labda kuna mnyama.

He! Nikamwona marehemu anapigana na mdogo wake Paulo. Nilivyoona hivyo mimi nikaona hawa si mtu na ndugu yake! Huyoooo nikapita zangu kurudi nyumbani, sikutaka hata kuwaangalia. Kesho yake nasikia eti Katandukila amefariki dunia, tena sehemu ile ile niliyokuta wanapigana na mdogo wake. Kwanza nikaona ninyamaze maana naweza kuonekana mwongo mimi." Ulikuwa ni ushuhuda wa Chambanenge.

Hata hivyo ulipingwa vikali na wanakijiji wengi wakiwamo ndugu wenyewe. Na iliaminika ni uongo kwa sababu ni mlevi. Yeye akiamka hafanyi kazi yoyote, kiguu na njia hadi kwenye kilabu cha pombe za kienyeji, kurudi zake nyumbani usiku wa manane.

Utakuwa mwenye bahati kubwa ukimwona mzima hajalewa. Muda wote yuko chakari. Hata wakati anatoa ushuhuda kikaoni alikuwa ameonja. Hilo lilimfanya asiaminike. Wako wachache walimwamini kutokana na mazingira ya kifo chenyewe. Waliunganisha matukio tu, wakaona Chambanenge yuko sahihi.

Kilichotokea ni kwamba huenda mwenyekiti alinyamazishwa na kushindwa kufuatilia tuhuma hizo, huku ndugu wa Paulo na Chambenenge nao wakihusika kwani waliona mmoja akikamatwa watakosa mwana na maji ya moto.

Yaani tayari wameshampoteza Chambanenge, halafu wampoteze pia Paulo aende kunyongwa, wakaona bora yaishe. Kikao cha siri cha wanandungu kilihusika kumaliza mkasa huo.

Kwenye vikao vya urithi, Paulo alianza kuonyesha chembechembe za yeye kuhusika na kifo cha kaka yake kwa kutaka yeye ndiye awe msimamzi wa mali yote, mke na mtoto pekee wa marehemu, Farida.

Mke wa Chambanenge alipinga kurithiwa na Paulo kwani aliona kwanza si utamaduni mzuri, lakini pia alikuwa na hasira naye kwa kuwa tayari kulikuwa na taarifa za tuhuma za kuhusika na kifo cha mumewe.

Kitendo cha kukataa ikawa balaa kwake. Akatimuliwa yeye na mtoto wake, huku akinyang'anywa mali zote za mumewe. Tabu alikimbilia kwa shangazi yake ambako ndiko alikoishi yeye na binti yake Farida.

Kutokana na maisha ya shida, wanachokula wanakijua wenyewe huku wakishindwa kabisa kupata haki yao kutokana na mfumo dume. Farida hakuendelea na shule tena baada ya kumaliza darasa la saba kutokana na hali mbaya ya maisha waliyokuwa nayo.

Kibaya zaidi mama yake, Tabu alifariki dunia na kumwacha na shangazi yake ambaye naye tayari alikuwa mtu mzima na asiyejiweza.

Akishirikiana na rafiki yake mmoja, waliamua kumtorosha Tabora na kwenda jijini Dar es Salaam kutafuta kazi. Kwa bahati nzuri walipata, kila mtu kwake.

Farida alipata bahati ya kupata kazi kama hausigeli katika nyumba ya Joel Kamagi maeneo ya Mbezi Louis, Dar es Salaam, ambaye alikuwa anajiweza kimaisha. Alikuwa na kampuni zake mbili za kusafirisha mizigo. Alikuwa na malori matano. Pia alikuwa na kiwanda cha kufyatua na kuuza matofali.

Pia alikuwa na hoteli moja maeneo ya Kisutu, Dar es Salaam. Akawa na zingine ndogo ndogo. Kifupi alikuwa mfanyabiashara mkubwa.

Kamagi alikuwa na mke na watoto watatu, wa kike wawili na wa kiume mmoja ambao kwa kiasi kikubwa walikuwa wanasoma mikoani wakikaa bweni, hivyo mara nyingi walikuwa hawaishi nyumbani mpaka likizo.

Farida alifanya kazi zake vizuri na kutokea kupendwa na waajiri wale. Miezi sita tu baada ya kuwa hapo, alinawiri na kupendeza kiasi cha kumvutia mwanamume yeyote yule mkware.

Miaka mitatu baadaye Farida alianza kubadilika. Alianza kuwa mvivu na kupenda kulala tu. Mama mwenye nyumba alipokagua vizuri akagundua kuwa tayari ameshakuwa mjamzito. Jambo hilo lilimshtua mama huyo. "Mimba ameipata wapi tena toba mtoto huyu wakati huwa hatoki hapa? Mbona hata sokoni anapelekwa na gari? Au dereva?" Akawaza mama mwenye nyumba.

"Atanieleza."

Siku aliyoamua kufanya hivyo ambapo hakuwapo mtu yeyote nyumbani alimwita chumbani kwake.

"Kaa hapo!" Akaambiwa kwa sauti ambayo Farida mwenyewe alijua haikuwa ya heri.

"Hebu niambie ukweli, usinifiche, wewe ni mjamzito au?"

Hakujibu chochote. Alionekana kushtushwa na swali lile.

"Si nakuuliza? Au hujasikia?"

"Nimesikia mama."

"Sasa mbona hunijibu?"

"Lakini mama..."

"Hakuna cha lakini, nataka jibu, una mimba huna?" Farida aliinama chini. Hakujua kama aseme ndiyo au hapana. Na hakujua jibu gani kati ya hayo mawili yatakayomtoa kwenye dhahama hiyo.

"Jibu wewe." Mama mwenye nyumba akimkumbusha kwa maneno na kuchapa kofi moja la kumtisha."

Itaendelea Jumapili

ITAENDELEA JUMAPILI



# BADO ANA HOFU

MWANAMUZIKI nyota kutoka Nigeria, Oluwatobiloba Daniel Anidugbe, maarufu kama Kizz Daniel ameibua mjadala baada ya kueleza kuwa tabia yake ya kuogopa kuchangamana na watu inatokana na unyanyasaji alioptia akiwa mtoto.

Amesema wakati alipokuwa mdogo alikuwa na unene kupita kiasi na kusababisha watoto wenzake kumcheka na kumdhihaki.


"Nimejenga ulimwengu wangu mwenyewe katika kichwa changu tangu nilipokuwa mdogo. Kwa sababu wakati nakua nilikuwa mtoto mnene. Nilikuwa mzito kiasi ambacho sikuweza kwenda nje nikihofia watoto katika eneo hilo watanidhihaki," amesema.

Amesema walimuita jina la orobo (mtu ambaye ni mnene) na walimdhulumu vitu vyake na kumfanya kukaa ndani kila wakati.

"Wakati huo ambao siku zote nilikaa ndani ya nyumba, tayari nilikuwa nimejenga ulimwengu huu wa ndoto kichwani mwangu, niko vizuri sana katika nafasi hiyo," amesisitiza.

Kizz Daniel aliongeza kuwa yeye hunywa pombe wakati mwingine ili kuweza kukabiliana na mahangaiko ya kijamii.

## *Tarisai kuitambulisha 'Addicted' Novemba*



MWIMBAJI wa muziki wa Injili mwenye asili ya Afrika anayeishi Australia, Tarisai Vushe, anatarajia kutambulisha kibao chake kipya 'Addicted' mwanzoni mwa Novemba.

Akizungumza na BT, Tarisai amesema wimbo huo unaobeba ujumbe wenye dhamira ya kumwabudu Mungu, unalenga kuhamasisha vijana kuwa na tabia ya kuabudu na kuachana na vitendo vya kishetani.

"Ninamshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya kumtumikia na sasa nipo tayari kuachia wimbo huu 'Addicted' ambao utatoka Novemba ukiwa katika mfumo wa audio na video. Huu ndio muda wa vijana kubadilisha maisha yao na kumgeukia Mungu," amesema Tarisai.

Aidha Tarisai amesema wimbo huo umechelewa kutoka kwa sababu alikuwa kwenye ziara ya kutoa huduma ya kiroho kwa watu mashuhuri kama William McDowell na Israel Houghton.

Tarisai ambaye ana asili ya Zimbabwe amesema lengo kubwa la kutangaza muziki wake Afrika ni uzalendo wake juu ya watu wa bara hilo.

Aliongeza kuwa anatamani kufanya kolabo na wanamuziki wa Tanzania kama Nandy kutokana na muziki wake kuwa wa kipekee.

## ZISIKUPITE

### DE GEA KUSTAAFU

GOLIKIPA wa Hispania, David de Gea, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Manchester United msimu wa joto, huenda akastaafu ikiwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 hatapokea ofa katika klabu kubwa. (***Guardian***)

### RONALDO AMSHAWISHI DE GEA

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 38 amekuwa akijaribu kumshawishi mchezaji mwenzake wa zamani wa Manchester United, David De Gea ajiunge naye Al Nassr lakini Mhispania huyo angependelea kubakia Ulaya. (***90 min***)

### ODEGAARD ALIKARIBIA SPURS

NAHODHA wa Arsenal, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 24 angeweza kujiunga na Tottenham Hotspur akiwa kijana lakini simu kutoka kwa gwiji wa Ufaransa, Zinedine Zidane ilimfanya kiungo huyo wa Norway kubadili mawazo. ***(Mirror)***

### LINGARD YUPO SAUDIA

KIUNGO wa zamani wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 30 atafanya mazoezi na Al-Ettifaq baada ya kuachwa na Nottingham Forest Juni na anaweza kujiunga na klabu hiyo ya Saudi Arabia kwa uhamisho wa bure. (Fabrizio Romano)

### FELIX ATAKIWA BEI JUU

BARCELONA inaamini Atletico Madrid itataka euro milioni 80 kubadilisha mkopo wa mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 23 katika klabu hiyo ya Nou Camp kuwa wa kudumu, wakati Manchester City wanataka euro milioni 25 kumuachia jumla Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 29. (***Mundo Deportivo***)

### CAMARDA AVUTIA

MSHAMBULIAJI wa AC Milan raia wa Italia, Francesco Camarda mwenye umri wa miaka 15 amezivutia Manchester City na Borussia Dortmund kwa mabao yake katika ngazi ya vijana. (***Calciomercato***)

### CAICEDO ALIITAKA CHELSEA

WAKALA wa kiungo wa kati wa Ecuador, Moises Caicedo amesema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 alitaka tu kujiunga na Chelsea msimu wa joto, licha ya Liverpool kutoa ofa ya pauni milioni 111 kumsajili kutoka Brighton. (***Sport Italia)***

### KLOPP ALIKATAA

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp alikataa ombi la kuwa kocha mpya wa Ujerumani kabla ya kumgeukia Julian Nagelsmann kuwaongoza kwa ajili ya Euro 2024. (***Telegraph)***

### DE LIGT AFADHAISHWA

MLINZI wa Uholanzi, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 24 amezidi kufadhaishwa na ukosefu wake wa kucheza katika kikosi cha kwanza katika klabu ya Bayern Munich msimu huu. (***Bild, via Mail***)

### ALCARAZ AFUATILIWA

NEWCASTLE United ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazomfuatilia kiungo wa kati wa Southampton raia wa Argentina, Carlos Alcaraz mwenye umri wa miaka 20. (***Sport)***

### CELSO AWANIWA

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo tayari kusikiliza ofa za kiungo mkabaji Giovani lo Celso mwenye umri wa miaka 27 Januari ingawa Muargentina huyo amepewa nafasi ya pili na kocha wa Spurs, Ange Postecoglou. (***Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA ASIFU UVUMILIVU WA KIPA RAMSDALE

**Baada ya kumuacha kama kipa namba moja na nafasi yake kuchukuliwa na...**

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amepongeza hatua ya mlinda mlango wa Arsenal, Aaron Ramsdale kukubali kuachwa na alikiri kuwa alipambana na uamuzi wa kumbadilisha na kumpa nafasi David Raya.

Arsenal walifanya uhamisho wa kushtukiza mwishoni mwa mwezi uliopita kumsajili Raya kutoka Brentford kwa mkopo wa awali wa msimu mmoja na chaguo la kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu licha ya Ramsdale kuimarika kama mlinda mlango wa klabu hiyo kiasi ambacho alizawadiwa kuongezewa muda mrefu.

**Raya ameanza mechi zote mbili za Arsenal tangu mapumziko ya kimataifa -- dhidi ya Everton wikendi iliyopita na ushindi wa kati kati ya juma Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya PSV Eindhoven.**

Arteta alisema bado hajaamua ni nani ataanza mechi ya leo Jumapili ya dabi ya London Kaskazini dhidi ya Tottenham Hotspur na alipoulizwa kama anajisikia vizuri kumuacha Ramsdale nje, alisema: "Labda naiangalia lakini tumboni mwako ukiwa na wachezaji wamekaa na unakuwa nao kutangaza safu, ni moja ya mambo magumu.

"Wachezaji wanahisi kuthaminiwa na kufurahi wanapocheza. Na wasipocheza ni ngumu sana. Unataka wajisikie kupendwa na kuaminiwa na njia ya kufanya hivyo ni kuwachezesha. Lakini kila mtu anaelewa kuwa ni mchezo wa timu na huwa ni wachezaji 11 wanaoanza.

"Lakini tumeona jinsi wamaliziaji walivyo muhimu, na jinsi kila mtu atakuwa muhimu katika msimu na sio kuangalia nyuma kwa timu ambayo imecheza mechi sita au saba za kwanza za msimu.

"Ni ngumu sana kwa kila mchezaji. Na ninateseka na ninajali kila mchezaji ambaye hachezi lakini huu ni ushindani na hii ni kazi yangu kufanya maamuzi kwa njia bora zaidi kwa timu.

"Amekuwa msaada mkubwa na mzuri sana mahali hapo na ndivyo ninatarajia kutoka kwa kila mchezaji kwani unapokuwa uwanjani kuna mtu mwingine hayupo, kwa hivyo inaenda pande zote mbili."

Arteta alilinganisha hali ya Ramsdale na Emile Smith Rowe, ambaye alifurahia katika Uwanja wa Emirates kama mbadala wa kipindi cha pili dhidi ya PSV baada ya kujipata kwenye kikosi cha kwanza msimu huu.

"Aaron ni mhusika wa kipekee, ana haiba hii na sote tunajua hilo na ninaelewa hilo kikamilifu," aliongeza Arteta.

"Inatokea kwa wachezaji wengine wengi, unaona mapokezi ambayo Emile alipata usiku uliopita na inatuma ujumbe kwamba tunampenda sana na ninampenda sana, na lazima tukabiliane na hilo."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI

ARSENAL
VERSUS
TOTTEHNAM

1 | 1.79
X | 4.03
2 | 4.13

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# DE GEA AKIKOSA TIMU ANASTAAFU

**RIYADH,** Saudi Arabia

DAVID de Gea anaweza kustaafu soka ikiwa hatapokea ofa ifaayo ya kurejea kwenye mchezo, huku akisisitiza kutokuwa tayari kwenda Ligi ya Saudia, vyanzo vimeithibitishia 90min.

Mhispania huyo bado hana klabu baada ya kuondoka Manchester United mwishoni mwa mkataba wake Juni mwaka huu.

Alikuwa ameafikiana kuhusu mkataba mpya, lakini Mashetani Wekundu waliondoa ofa yao ya awali na kushindwa kukamilisha mkataba mpya.

90min iliripotiwa katika majira ya joto kwamba Bayern Munich na Real Madrid zilijadili uhamisho wa De Gea, ingawa hakuna hata mmoja aliyetuma ofa kwa kipa huyo.

Licha ya kuwaniwa na Klabu za Saudi Pro League na Qatari Stars League, 90min anaelewa kuwa De Gea angependelea kusalia Ulaya na ameweka wazi hilo kwa washiriki wanaovutiwa kutoka Mashariki ya Kati.

Mchezaji mwenzake wa zamani wa Man Utd, Cristiano Ronaldo amekuwa akijaribu kumshawishi De Gea ajiunge naye Al Nassr, lakini kipa huyo habadiliki na msimamo wake wa sasa.

De Gea ana nia ya kucheza soka la Ligi ya Mabingwa Ulaya na yuko tayari kusubiri hadi dirisha la uhamisho la Januari litakapofunguliwa ili kuamua juu ya uhamisho wake mwingine.


Hata hivyo, ikiwa hatapokea 'ofa sahihi', vyanzo vimeiambia 90min kwamba De Gea atafikiria kustaafu.

De Gea, ambaye anatimiza umri wa miaka 33 Novemba, ametumia maisha yake yote hadi kufikia hatua hii akiwa na klabu mbili pekee - Atletico Madrid na kisha Man Utd.

Hajaichezea timu ya taifa ya Hispania tangu 2020 na aliachwa nje ya kikosi chao kwa Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

Mrithi wake katika klabu ya Man Utd, Andre Onana, amekuwa na mwanzo mbaya wa maisha pale Old Trafford, hivi majuzi zaidi akiruhusu bao wakati wa kichapo cha 4-3 kutoka kwa Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano.

# Silva kurejea dimbani wiki ijayo



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anatarajia Bernardo Silva atarejea uwanjani wiki ijayo baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno kuumia kwenye mchezo wa Ligi ya mabingwa Ulaya Jumanne iliyopita.

Silva aliondoka kwenye mchezo muda mfupi kabla ya kipindi cha mapumziko baada ya kupata bao, na kuongeza jina lake kwenye orodha ya majeruhi pale City.

"Tuko taabani lakini sitasema, 'Ah, tuna majeraha mengi'," alisema Guardiola baada ya ushindi huo wa 3-1.

"Tunapokuwa na wachezaji watano muhimu - wachezaji muhimu sana - waliojeruhiwa, kudumisha hilo kwa muda mrefu itakuwa vigumu. Lakini ndivyo ilivyo."

Kwa bahati nzuri, inaonekana kana kwamba Silva anaweza kurejea uwanjani punde tu Guardiola alipotoa kauli chanya wakati wa mkutano na waandishi jana.

"Ni jeraha kidogo, kwa wiki - siku kumi atakuwa nje," alifichukua Guardiola.

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# SINGIDA FG KUIFUATA FUTURE FC SEPT 27

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha timu ya Singida Fountain Gate kinatarajiwa kwenda Misri Septemba 27 tayari kwa mchezo wao wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Future FC ya nchini humo.

Singida inatarajiwa kurudiana na Wamisri hao Oktoba Mosi mchezo utakaotoa majibu ya nani anatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa habari wa klabu hiyo, Hussein Masanza alisema utaratibu wa safari hiyo unaendelea na upo kwenye hatua za mwisho lakini pia maandalizi ya timu kuelekea kwenye mchezo huo yanaendelea.

"Leo( jana) tumeanza mazoezi rasmi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wetu wa marudiano wa kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi ya Future FC, mchezo utachezwa Oktoba Mosi, benchi la ufundi linaendelea kukiandaa kikosi huku kikiwa na shauku ya kuifikisha timu kwenye hatua ya makundi," alisema Masanza.

Alisema kama mambo yataenda sawa wamepanga kusafiri na kikiosi cha wachezaji 24, benchi la ufundi na baadhi ya viongozi lengo ni kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kucheza hatua ya makundi.

"Kila mchezaji ana morali ya kwenda kupambana kuhakikisha wanawapa burudani watanzania kwa kushinda mchezo huo na kuingia hatua ya makundi, hili ndilo lengo letu hasa baada ya kumalizika kwa mchezo wetu wa kwanza ambao tulipata ushindi hapa nyumbani," alisema Masanza.

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa kwenye uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Singida FG ilifanikiwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0, matokeo hayo yanaifanya Singida FG kwenda kusaka ushindi au sare yoyote kuweza kutinga hatua hiyo ya makundi.




Meneja wa Wateja Maalum wa Tigo Pesa, Mary Rutta (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi mshindi wa shindano la Tigo Cha Wote, Devotha Kweka, katika hafla iliyofanyika juzi jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tigo yaneemesha washindi 28,600

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya washindi 28,600, wamejishindia zawadi ya fedha Sh. milioni moja kila mmoja kwenye kampeni ya Tigo ya Cha Wote iliyomalizika juzi nchi nzima.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi kwa washindi hao jijini Dar es Salaam juzi, Meneja wa Wateja Maalum wa kampuni hiyo, Mary Rutta, alisema zaidi ya washindi 28,600 tayari walishapatikana na kupatiwa zawadi zao.

Alisema kampeni hiyo imedumu kwa kipindi cha siku 90 ambapo mbali na fedha taslim, wamekuwa wakitoa bonasi, dakika na intaneti kwa washiriki wa shindano hilo.

"Leo tunayo furaha kubwa kuwa na baadhi ya washindi wa shindano la Cha Wote, ambao hawa ni washindi wa fedha kila mmoja.

"Kampeni ya shindano la Tigo Cha Wote imefikia tamati baada ya kufanyika kwa kipindi cha siku 90, washindi zaidi ya 28,600 nchi nzima wamepatikana na kukabidhiwa zawadi zao," alisema.

Alisema anawaomba wadau mbalimbali kuendelea kutumia mtandao wa Tigo, kuhakikisha wanajishindia zawadi mbalimbali kila kipindi wanapotangaza kampeni zao.

Mshindi Devotha Kweka kutokea Dar es Salaam ambaye alijishindia zawadi ya fedha alisema anatarajia kutumia fedha hizo kukuza biashara yake na mambo yake binafsi.

"Nimefurahia kuwa mmoja wa washindi wa shindano la Tigo Cha Wote kwa mwaka huu, ninatarajia kutumia fedha hizo kukuzia biashara zangu na mambo binafsi.

"Nilikuwa nikifanya miamala mbalimbali kupitia simu ya mkononi na kuwa miongoni mwa washindi, hivyo ninatarajia kuendelea kucheza mashindano mengine yatakayotangazwa ili niendelee kujishindia zawadi," alisema.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 24/09/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 4497 | Sparta Rotterdam vs Vitesse Arnhem | 1.88 | 3.56 | 3.61 |
| 13:30 | 3167 | Empoli vs Inter | 7.41 | 4.94 | 1.40 |
| 14:00 | 1735 | Stoke City vs Hull City | 1.87 | 3.62 | 3.57 |
| 14:00 | 5202 | Metz vs Strasbourg | 2.89 | 3.25 | 2.52 |
| 14:30 | 4108 | Kaiserslautern vs Hansa | 2.00 | 3.40 | 3.50 |
| 14:30 | 4188 | Holstein Kiel vs Hertha BSC | 2.55 | 3.60 | 2.44 |
| 14:30 | 4320 | Fortuna Dusseldorf vs Hannover | 1.86 | 3.74 | 3.64 |
| 14:30 | 4624 | Racing Genk vs St Truiden | 1.56 | 4.10 | 5.00 |
| 15:00 | 1782 | Real Sociedad vs Getafe | 1.59 | 3.70 | 6.58 |
| 15:00 | 3172 | Silkeborg vs Viborg FF | 1.98 | 3.72 | 3.32 |
| 15:30 | 5296 | Ajax vs Feyenoord | 2.67 | 3.56 | 2.30 |
| 16:00 | 1628 | Brighton vs Bournemouth | 1.45 | 5.01 | 6.16 |
| 16:00 | 2118 | Chelsea vs Aston Villa | 2.00 | 3.67 | 3.62 |
| 16:00 | 2608 | Udinese vs Fiorentina | 3.10 | 3.46 | 2.28 |
| 16:00 | 2622 | Arsenal vs Tottenham | 1.79 | 4.03 | 4.13 |
| 16:00 | 2769 | Lens vs Toulouse | 1.72 | 3.95 | 4.62 |
| 16:00 | 2823 | Liverpool vs West Ham | 1.46 | 4.99 | 6.14 |
| 16:00 | 3374 | Atalanta vs Cagliari | 1.42 | 4.84 | 7.20 |
| 16:00 | 4829 | Orlando Pirates vs Stellenbosch | 1.70 | 3.28 | 4.64 |
| 16:00 | 5145 | Le Havre vs Clermont Foot | 2.44 | 3.28 | 2.98 |
| 16:30 | 4599 | Bayer Leverkusen vs Heidenheim | 1.26 | 6.37 | 9.86 |
| 16:30 | 5610 | Zenit St Petersburg vs Lokomotiv Moscow | 1.42 | 4.52 | 6.16 |
| 17:00 | 3263 | Aberdeen vs Ross County | 1.92 | 3.43 | 3.68 |
| 17:00 | 4029 | Cercle Brugge vs Union Saint Gilloise | 2.64 | 3.38 | 2.44 |
| 17:00 | 4574 | Besiktas vs Kayserispor | 1.38 | 4.65 | 6.81 |
| 17:00 | 5054 | Rangers vs Motherwell | 1.21 | 5.96 | 10.92 |
| 17:00 | 5567 | Sunderland vs Cardiff | 1.83 | 3.52 | 3.87 |
| 17:15 | 2269 | Rayo Vallecano vs Villarreal | 2.50 | 3.54 | 2.72 |
| 17:15 | 3673 | Real Oviedo vs Valladolid | 2.44 | 2.82 | 3.07 |
| 17:15 | 3968 | Parma vs Sampdoria | 2.14 | 3.24 | 3.19 |
| 17:30 | 1245 | GD Chaves vs CF Estrela | 2.49 | 3.29 | 2.64 |
| 17:30 | 2963 | BSC Young Boys vs FC Lugano | 1.58 | 4.13 | 4.75 |
| 17:45 | 2354 | PEC Zwolle vs AZ Alkmaar | 4.26 | 3.82 | 1.69 |
| 17:45 | 4125 | Waalwick vs Twente | 5.14 | 4.45 | 1.49 |
| 18:05 | 2254 | Montpellier vs Rennes | 2.67 | 3.54 | 2.55 |
| 18:30 | 2073 | Eintracht Frankfurt vs SC Freiburg | 2.09 | 3.60 | 3.40 |
| 18:30 | 3900 | Sheffield Utd vs Newcastle | 6.37 | 4.62 | 1.48 |
| 19:00 | 1083 | Bologna vs Napoli | 3.58 | 3.53 | 2.05 |
| 19:00 | 1979 | Midtjylland vs Odense | 1.57 | 4.14 | 5.05 |
| 19:30 | 1394 | Betis vs Cadiz CF | 1.85 | 3.53 | 4.40 |
| 19:30 | 3752 | Anderlecht vs Brugge | 2.94 | 3.54 | 2.16 |
| 19:30 | 4411 | Mirandes vs Leganes | 2.52 | 2.91 | 2.86 |
| 19:30 | 4475 | Las Palmas UD vs Granada | 2.03 | 3.49 | 3.69 |
| 20:00 | 1817 | Alanyaspor vs Fenerbahce | 4.74 | 3.86 | 1.63 |
| 20:00 | 5665 | Portimonense vs Benfica | 9.76 | 5.78 | 1.24 |
| 20:15 | 1468 | KAA Gent vs Eupen | 1.26 | 5.55 | 9.11 |
| 21:45 | 1781 | Paris St Germain vs Marseille | 1.78 | 3.94 | 4.24 |
| 21:45 | 5175 | Torino vs Roma | 3.07 | 3.02 | 2.54 |
| 22:00 | 5520 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 2.70 | 3.31 | 2.64 |
| 22:30 | 2158 | Sporting Braga vs Boavista | 1.50 | 4.18 | 5.57 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Septemba 24, 2023
Nipashe



De Gea akikosa timu anastaafu UK. 22

# Gamondi ataka mabao mengi kwa Al Merrikh



**●●●Aifungia kazi safu yake ya ushambuliaji, awapa majukumu mazito Mzize, Musonda kuhakikisha wana...**

**Na Saada Akida**

IKIWA imebaki wiki moja kabla ya mchezo wa marudiano wa ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi ameifungia kazi safu yake ya ushambuliaji kwa kuinoa ili impe mabao mengi kwenye mchezo huo dhidi ya Al Merrikh ya Sudan utakaochezwa Septemba 30 kwenye uwanja wa Azam Complex.

Gamondi, amesema licha ya ushindi wa mabao 2-0 walioupata kwenye mchezo wa kwanza ugenini, bado ana kiu ya kupata mabao mengi kwenye mchezo wa nyumbani na jambo hilo linawezekana kama wachezaji wake watatumia vizuri nafasi watakazozitengeneza.

"Tulitengeneza nafasi nyingi sana mchezo uliopita lakini hatukuzitumia, nimewapa washambuliaji wangu, Mzize na Musonda kuhakikisha tunatumia vizuri nafasi tunazozitengeneza, sitaki kuyaona yale ya mchezo uliopita, tulikuwa na nafasi ya kupata mabao mengi lakini hatukutumia nafasi," alisema Gamondi.

Aidha, alisema anaendelea kwanoa washambuliaji wake hao ili waweze kuwa na uwezo wa kutumia vizuri nafasi nyingi ambazo wamekuwa wakizitengeneza.

"Tunahitaji mabao mengi zaidi katika mchezo ujao maana kila timu inahitaji ushindi katika hatua hiyo kuweza kufuzu hatua ya makundi, Wenzetu walipoteza mchezo wa kwanza, naamini watakaporudi uwanjani tena watarudi kivingine kuhakikisha wanapata ushindi, tunatakiwa kwenda kupambana kuweza kupata matokeo, tuna nafasi ya kupata ushindi, nataka ushindi wa mabao mengi" alisema kocha huyo.

**Gamondi alisema ameona changamoto ya kikosi chake kwenye safu ya ushambuliaji kutotumia vizuri nafasi wanazotengeneza akitolea mfano mchezo uliopita wa ligi kuu dhidi ya Namungo FC ambao Yanga licha ya kumiliki mpira na kutengeneza nafasi nyingi, walipata ushindi 'kiduchu' wa bao 1-0.**

"Hakuna mechi rahisi lakini tunatakiwa kuwa makini na utulivu katika kutumia nafasi tunazotengeneza ili kupata ushindi mzuri, ninaimani Al Merrikh watakuja tofauti na mechi ya kwanza na kama tumeweza kupata ushindi kwao, tusipokuwa makini kama mchezo wetu na Namungo tutajiweka kwenye nafasi ngumu, wapinzani wetu pia wana uwezo wa kupata ushindi ugenini," alisema Kocha huyo.

Aidha, kocha huyo amesema anaangalia uwezekano kama kutakuwa na nafasi ya kupata mchezo mmoja wa kirafiki kuelekea kwenye mchezo huo.

Yanga imefika hatua ya kuwania kutinga makundi baada ya kupata ushindi wa jumla wa mabao 7-1 dhidi ya Asas FC ya Djibouti katika hatua ya kwanza ya mtoano ya mashindano hayo.

Msimu uliopita Yanga ilikuwa mshindi wa pili wa Kombe la Shirikisho Afrika (CAFCC), nyuma ya mabingwa USM Alger ya Algeria na kukosa taji hilo kwa kanuni ya bao la ugenini, ambapo walifungwa mabao 2-1 nyumbani na wakashinda 1-0 ugenini.

Yanga iliangukia katika Kombe la Shirikisho baada ya kutolewa katika Ligi ya Mabingwa Afrika kufuatia kipigo cha jumla ya mabao 2-1 dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

## Simba SC yaifungia kazi Power Dynamos

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba kimeingia kambini juzi kujiandaa na mechi ya mkondo wa pili ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia utakaochezwa Jumapili ijayo (Oktoba Mosi) Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Kikosi hicho kimeingia kambini baada ya mapumziko ya siku moja tangu ilipocheza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union Alhamisi iliyopita na kushinda mabao 3-0.

Katika mazoezi ya jana kwenye Uwanja wa Mo Arena, Bunju, Dar es Salaam, wachezaji wa timu hiyo walionekana kugawanyika sehemu mbili, waliocheza dakika zote mechi ya Alhamisi waliwekwa kwenye kundi lao na wale waliocheza kwa dakika chache na wale ambao hawakucheza kabisa waliwekwa kwenye kundi lao na kuanza mazoezi kabla ya kucheza mchezo wa wenyewe kwa wenyewe.

Makundi hayo mawili yalikuwa yakisimamiwa na kocha wa viungo, Corneille Hategikimana na Kocha Roberto Oliviera 'Robertinho'. Akizungumza na gazeti hili, Robertinho alisema wameanza rasmi kujiandaa na mchezo dhidi ya Power Dynamos na mazoezi yao yote ni kuelekea kwenye mchezo huo muhimu ambao wanahitaji ushindi tu.

"Tumeanza na programu maalum kwa wachezaji wote kwa kuvigawa katika makundi mawili, lakini kiujumla tumeanza kujiandaa na mchezo wetu wa mrudiano, tunataka kuona tunaingia hatua ya makundi," alisema Robertinho.

Aidha, alisema wapinzani wao si timu dhaifu na watakuja kwa nguvu kujaribu kulazimisha ushindi au sare yenye manufaa kwao.

"Mchezo hautakuwa mwepesi, lakini nina imani na wachezaji wangu ingawa nitamkosa Inonga (Henock), lakini waliobaki wanaweza wakanipa kile ambacho nakitaka na mashabiki wanachokisubiria," alisema Robertinho.

Inonga ataukosa mchezo huo baada ya kuumia kwenye mchezo wa ligi kuu dhidi ya Coastal union na anatarajiwa kuwa nje kwa wiki mbili.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >